# Nipashe

Jumanne Juni 16, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580259

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Tanga yatajwa kinara matukio ukatili wa watoto

UKURASA 4




UKURASA 11

# Mbio kumrithi Shein kishindo

- Mtoto wa Karume aja na vipaumbele kibao... Endelea Uk. 2




Balozi Ali Amani Karume akionyesha mkoba wenye fomu ya kuomba kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), baada ya kukabidhiwa katika Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**.

## SERIKALI YATETEA KUPOKA MAPATO YA HIFADHI

UKURASA 3

## Magufuli kulifunga Bunge leo

- *Wapinzani waunga mkono Bajeti 2020/21*

UK. 2

## BAA LA CORONA



Chakula kinaweza kupikwa kwa muda gani kujikinga na virusi vya corona? Jibu ni kwamba virusi hivi havistahimili joto kama vilivyo virusi vingine na bakteria wanaopatikana kwenye chakula. Hata hivyo, ili kuwa salama chakula kipikwe angalau kwa nyuzijoto 70 kama inavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO)

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** SIMBA SC YAKATAA KUTUPIANA LAWAMA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM kufunga Bunge leo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RAIS John Magufuli leo atakuwa bungeni kwa ajili ya kulifunga Bunge la 11 alilofungua Novemba 20, 2015.

Pamoja na mambo mengine, hotuba ya Rais itajielekeza zaidi kueleza mambo mbalimbali ambayo serikali yake imeyatekeleza kwa kipindi cha miaka mitano ambayo yameainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-20.

Kufungwa kwa bunge hilo maana yake ni kuwa limemaliza uhai wake wa miaka mitano, hivyo wabunge wanaomaliza muda wao na wanataka kurejea tena sasa wanakwenda katika mchakato wa vyama vyao kwa ajili ya kuteuliwa ili kugombea tena katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Wale ambao wameshatangaza kutogombea tena watakuwa wamekamilisha jukumu la kuwawakilisha wananchi wao bungeni.

Wabunge waliokwishatangaza kutogombea tena ni Prof. Anna Tibaijuka (Muleba Kusini-CCM); Sadifa Hamis Juma (Donge-CCM) na Wilfred Lwakatare (Bukoba Mjini-Chadema).

**BAJETI YAPITA KWA KISHINDO**

Wakati huo huo, Bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, imepitishwa na Bunge baada ya wabunge 304 kupiga kura ya 'Ndiyo' huku 63 wakipiga kura ya 'Hapana'.

Kwa mujibu wa matokeo ya kura hiyo ambayo kila mbunge alihojiwa, kura zote zilizopigwa zilikuwa 371, huku safari hii wabunge wengi zaidi wa baadhi ya vyama vya upinzani wakiipigia kura ya 'Ndiyo'.

Baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo, Spika Job Ndugai aliyekuwa anaongoza kikao, aliyaelezea kuwa ni ya kihistoria, akibainisha kuwa hiyo ni bajeti iliyopigiwa kura nyingi zaidi za 'Ndiyo' katika Bunge la 11 linalotarajiwa kufungwa leo.

Vyama viwili kati ya vinne vya upinzani vyenye uwakilishi bungeni wabunge wake walitofautiana katika kupiga kura ya kuamua ama kupitishwa au kutopitishwa kwa bajeti hiyo ya Sh. trilioni 34.88.

Vyama hivyo ni CUF na Chadema. Zitto Kabwe, kiongozi na mbunge pekee wa Chama cha ACT-Wazalendo, na James Mbatia, kiongozi na mbunge na kiongozi wa NCCR-Mageuzi walipiga kura ya 'Hapana'.

Baadhi ya wabunge wa upinzani waliopiga kura ya 'Ndiyo' kwa bajeti hiyo ya serikali ni pamoja na Magdalena Sakaya (Kaliua) na Maftaha Nachuma (Mtwara Mjini), wote wakiwa viongozi wa CUF pia.

Wengine ni Sonia Magogo (Viti Maalum - CUF) na wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) waliotangaza kukihama chama hicho, wakiongozwa na Peter Lijualikali, Mbunge wa Kilombero.

# Makada wawili wajitosa urais CCM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADA ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kufungua milango ya kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar, wanachama wawili jana walijitokeza kuchukua fomu ya kugombea nafasi hiyo.

Mmoja ni mtoto wa Rais wa kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume, alikuwa mwanachama wa pili kuchukua fomu akifuatiwa na Mbwana Juma Bakari (45).

Uchukuaji wa fomu ulifanyika katika Ofisi Kuu za CCM Kisiwandui Mjini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari Balozi Ali Karume alisema CCM haina ubaguzi na miongoni mwa vigezo wanavyoangalia ni uwezo wa kiutendaji ambacho anacho.

Alisema iwapo atateuliwa na kupata ridhaa ya wananchi ataendeleza dhamira ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuyalinda, kulinda Muungano na kuendeleza sera za CCM.

Alieleza kuwa Rais anayemaliza muda wake, Dk. Ali Mohamed Shein, ameshirikiana na Baraza la Mapinduzi na kufanya kazi ya kupigiwa mfano katika kuendeleza sera zilizoainishwa na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Mzee Abeid Amani Karume.

Balozi Karume alisema nia yake ni kuyaendeleza yote mazuri yakiwamo afya na elimu bure, ugawaji wa ardhi kwa wananchi na ujenzi wa makazi bora.

Alieleza kuwa ipo haja ya kuleta usawa wa kijinsia, kuwalinda watoto, kuwatunza wazee na kuwapa vijana elimu ya kujitegemea.

"Ujamaa, udugu, upendo na mshikamano ndio ngao zetu...nakuombeni nyote mniombee kwa mwenyezi Mungu na tuiombe nchi yetu na jamii zetu Mungu atujalie tuendelee kuwa na hali ya usalama, amani na utulivu," alisema Balozi Karume.

Balozi Karume ni Waziri wa Vijana, Sanaa, Michezo na Utamaduni na kwa zaidi ya miaka 30 amekuwa balozi wa Tanzania katika nchi mbalimbali za Ulaya na Amerika ikiwamo Ujerumani, Italia, Ubelgiji na Marekani.

Baada ya kuchukua fomu hiyo Balozi Karume alipata nafasi ya kuzuru kaburi la muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, Hayati Abeid Amani Karume, ambaye ni baba yake mzazi.

Hii ni mara ya tatu kwa Balozi Karume kuomba ridhaa ya CCM kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar, ambapo mwaka 2015 alichukua fomu kuomba ridhaa kugombea nafasi ya urais kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwaka 2010 alichukua fomu ya kugombea urais wa Zanzibar.

**MBWANA BAKARI JUMA**

Naye mgombea Mbwana Bakari Juma ambaye ni maarufu katika duru za kisiasa Zanzibar, aliahidi kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kuigeuza Zanzibar kuwa kituo kikuu cha biashara cha kimataifa.

Juma ambaye ni muhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam mwaka 1999, alisema Zanzibar ni kitovu cha biashara tangu kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, huku ikiwa kiungo muhimu cha nchi za Afrika hadi Bara la Hindi na Ulaya.

''Nimechukua fomu kwa ajili ya kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kuongoza Zanzibar...nimejipanga kuleta mabadiliko makubwa na kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha biashara katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Bara la Hindi hadi Ulaya," alisema.

Wanachama hao walikabidhiwa fomu na Katibu wa Idara ya Organization ya Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM Zanzibar, Galouis Nyimbo.




Katibu wa NEC, Idara ya Oganizesheni ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Cassian Galos Nyimbo (kushoto), akimkabidhi mkoba wenye fomu mwanachama wa chama hicho, Mbwana Bakari Juma, aliyejitokeza kuwania urais kupitia CCM, mjini, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**.

# Bwege atimkia ACT-Wazalendo

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Kilwa Kusini (CUF), Selemani Bungura, amefichua mazungumzo yake na Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, kabla ya kufikia uamuzi wa kuhamia katika chama hicho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, mbunge huyo alisema alikwishafahamu kuwa katika mgogoro ulioikumba CUF, ulihusisha waliomuunga mkono aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif na waliokuwa wakimuunga mkono, Prof. Ibrahimu Lipumba, upande wa Lipumba ndio ungeshinda kwa madai ya kutumiwa na dola.

"Mimi nilijua mapema kuwa hii vita kati ya Maalim na Lipumba, Maalim Seif hawezi kushinda iwe haki yake au siyo haki yake kwa hiyo nilishaongea na Zitto siku nyingi inawezekana Maalim ndio amenifuata mimi," alisema Bungara.

Alisema baada ya Bunge kuvunjwa atahamia rasmi ACT-Wazalendo na akipewa ridhaa atagombea tena nafasi hiyo ya ubunge katika Jimbo la Kilwa Kusini, huku akitamba kuwa ataibuka mshindi katika uchaguzi huo kwa kile alichodai kuwa ACT-Wazalendo ndio chama kikuu cha upinzani kwa sasa katika jimbo hilo.

Akiongelea kuhusu utofauti wa kiitikadi kati ya CUF alichotoka na ACT-Wazalendo alichohamia, alisema vyama vya siasa vyote havifuati itikadi zao ikiwamo na kwamba atakapohamia katika ACT-Wazalendo atahakikisha kuwa anasimamia kufuatwa kwa itikadi ya chama na misingi ya uadilifu kwa viongozi.

Bungara ni mbunge wa kwanza wa kuchaguliwa kutoka Tanzania Bara kutangaza kuhamia ACT-Wazalendo baada ya mgogoro ulikuwapo CUF na kusababisha makada wengi wa chama hicho akiwamo aliyekuwa Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif kutimkia ACT-Wazalendo.

HABARI KITAIFA

# Serikali yatetea uamuzi kupoka mapato ya Tanapa, Ngorongoro

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imetetea uamuzi wake wa kukusanya maduhuli yanayokusanywa na Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori (Tawa).

Kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2020, uliowasilishwa bungeni jijini hapa jana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, serikali inakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sura 282, ili kuipa Mamlaka ya Mapato (TRA) mamlaka kisheria kukusanya maduhuli ambayo sasa yanakusanywa na Tanapa, NCAA na Tawa.

Zitto Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), akichangia muswada huo, alipinga vikali uamuzi huo, akitahadharisha kutokea tatizo la kiuchumi kwa Serikali Kuu kuingilia utendaji wa mamlaka za kiutalii kama ilivyokuwa kwenye zao la korosho miaka miwili iliyopita.

Mtaalamu huyo wa uchumi aliikumbusha serikali kuwa sekta ya utalii kwa sasa inachangia asilimia 27 ya fedha zote za kigeni nchini, hivyo uamuzi wowote unaochukuliwa dhidi ya sekta hiyo unapaswa kufanyika baada ya kufanya tathmini ya kina ya madhara yake.

Alisema anashangazwa na kile alichokiita utaratibu mpya wa serikali kutia mkono kwenye kila eneo inaloona lina fedha nyingi na kulipoka mamlaka ya kukusanya.

Katika majibu yake kwa suala hilo, Dk. Mpango, alisema dhamira ya serikali kamwe haiwezi kuua uhifadhi, lakini imefikia uamuzi wa kupoka mapato ya mamlaka hizo tatu baada ya kubaini mapato yake hayadhibitiwi vizuri na kwamba kipindi hiki cha mlipuko wa corona zimeshindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi wake zaidi ya 3,000.

Alisema kupitia ukaguzi mbalimbali, wamegundua kwamba mamlaka hizo za hifadhi zina upungufu mkubwa ikiwamo uhaba wa wafanyakazi.

Waziri Mpango alisema Hazina, Wizara ya Maliasili na Utalii na mamlaka za hifadhi zitakaa pamoja kuandaa taratibu za kuhakikisha kwamba shughuli nyeti za uhifadhi zinafanyika ikiwa ni pamoja za operesheni za dharura kukabiliana na ujangili.

"Tutafanya hivyo kama ambavyo tunafanya pia kwa ajili ya vyombo vya ulinzi na usalama vingine vyote ambavyo posho zao zinalindwa, na utaratibu huu siyo mpya, ndiyo unaotumika TRA, lakini pia unatumika, jeshi hawajawahi kulalamika kuhusu posho zao, mifuko yote, Mamlaka za Viwanja vya Ndege na unatumika kwa ufanisi," alisema.

Alisema kwa sasa serikali itachukua jukumu la kulipa mishahara ya watumishi wa mamlaka hizo na kutekelezaji miradi yake, ikiwa ni pamoja na ukarabati wa miundominu.

Alisema wamebaini siyo sawa watumishi zaidi ya 3,000 walioko kwenye mamlaka hizo tatu kuwa nje ya malipo ya mishahara ya serikali na kushindwa kulipwa mishahara kipindi hiki cha corona.

Waziri Mpango pia alisema serikali itaendelea kufuatilia mwenendo wa viashiria vya uchumi na utekelezaji wa bajeti kwa ujumla na kama itabainika kutakuwa na haja ya kufanya marekebisho ya bajeti, itafanya hivyo wakati wa mapitio ya nusu mwaka Desemba mwaka huu.

**UTAKATISHAJI**

Dk. Mpango pia alisema muswada huo unapendekeza kurekebisha vifungu vya 3 na 15 vya Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu, Sura 423, ili kumtambua ndani ya sheria mnufaika wa mwisho kwa lengo la kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa.

Pia, kuhakikisha taarifa sahihi za wanufaika wa mwisho zinapatikana, zinathibitishwa, zinahifadhiwa na kutambulika, ili kusaidia udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 15/06/2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI tarehe 20/06/2020** kampuni ya **SINO-SHINE OVERSEAS CONSTRUCTION & INVESTMENT (EA) LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **INYONGA kuelekea KABANGA kupitia TABORA**, Gari hilo yana namba za usajili: **T 550 BES/T474 BCJ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **16** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.6** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.9** |

3. Njia itakayotumika: **INYONGA hadi KABANGA** kupitia TABORA Gari litasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115774602


## Nacte yafungua dirisha usajili wanavyuo

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Taifa la Elimu ya Ufundi (Nacte), limefungua milango ya udahili wa wanafunzi katika ngazi ya astashahada na stashahada kwa kozi zote zinazotolewa na vyuo vya elimu ya ufundi kuanzia jana hadi Septemba 15, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Uthibiti, Ufuatiliaji na Tathmini wa Nacte, Jofrey Oleke, alitangaza kuanza kwa usajili huo jana jijini Dar es Salaam kuwa vyuo vinaruhusiwa kuanza kupokea maombi ya wanafunzi kuanzia jana hadi Septemba 15, mwaka huu.

Alisema vyuo hivyo vitachagua waombaji wenye sifa kati ya Septemba 21 na kuanzia Septemba 22 hadi 29, mwaka huu, majina ya waombaji waliochaguliwa yatawasilishwa Nacte kwa ajili ya uhakiki.

Oleke alisema majina ya waliochaguliwa na kuhakikiwa na Nacte yatatangazwa na vyuo husika Oktoba 8, mwaka huu, kwa ajili ya kuanza masomo Novemba 16, mwaka huu.

Kadhalika, alisema waombaji wa programu za afya kwenye vyuo vya serikali watatuma maombi yao moja kwa moja kupitia tovuti ya Nacte kuanzia Juni 15 hadi Agosti 15, mwaka huu.

Alisema majina ya watakaochaguliwa yatatangazwa Agosti 26, mwaka huu na vyuo vyote vya elimu ya ufundi vitakavyopokea maombi ya wanafunzi ya ngazi ya astashahada na stashahada kuanzia jana, mwaka huu, vitaelekezwa kuzingatia taratibu za udahili kama zilivyotolewa na Nacte kwa mwaka wa masomo ya mwaka 2020/21.

Alisema wahitimu wote wa elimu ya sekondari na vyuo wenye sifa za kujiunga na kozi za astashada na stashahada, wanashauriwa kufanya maombi yao kwa umakini ili kupata nafasi ya kujiunga na kozi wanazozipenda na wanatimiza vigezo za kujiunga nazo kwa mwaka wa masomo 2020/21.

Oleke aliwashauri waombaji na wazazi kuhakikisha kuwa wanaomba vyuo ambavyo vimeorodheshwa kwenye kitabu cha mwongozo wa udahili kwa mwaka wa masomo 2020/21 unaopatikana kwenye tovuti yao.

Alisema, vyuo vyote vilivyofutiwa usajili au kufungwa havitatakiwa kusajili wanafunzi wapya hadi hapo watakapokamilisha taratibu za Nacte.



Mkandarasi akiendelea na ujenzi wa kingo za Mto Ng'ombe, katika eneo la Tandale jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UWEKAJI WAZI DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi kuwa itaweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa siku nne kuanzia tarehe **17 hadi 20 /06/2020,** katika vituo vilivyotumika wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga Kura.
Uwekaji wazi huu utafanyika kwa kuzingatia tahadhari zote za afya kuhusu kuzuia maambukizi ya ugonjwawa COVID-19 unaosababishwa na Virusi vya Corona.

Uboreshaji utafanyika kama ifuatavyo :-

1. **SIKU** : Uwekaji wazi utafanyika tarehe 17-20/06/2020
2. **VITUO** : Uwekaji Wazi utafanyika katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Halmashauri husika.
3. **MUDA** : Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uwekaji Wazi utahusisha.**

- Wapiga Kura wote walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mwaka 2015, walioandikishwa wakati wa Uboreshajiwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na ya Pili kwa Mwaka 2019/2020.
- Wapiga Kura hawa ni wale ambao hawakuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura awamu ya kwanza.
- Wapiga kura watakaohakiki taarifa zao kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura lilipowekwa wazi na kukuta picha zao hazipo wanatakiwa kwenda kwenye ofisi za Halimashauri ili wapigwe picha nyingine na kupewa kadi..
- Kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam wakazi wa Kata za Kipawa kituo cha Ofisi ya Weo Kipawa 'A' katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala , na kituo cha shule ya Msing Mwongozo 'B' kata ya Mwananyamala katika Halimashauri ya Manispaa ya Kinondoni , Wote wanatakiwa waende katika vituo hivyo ili kukamilisha taarifa zao katika kanzi data

**Utaratibu wa Uhakiki.**
Mpiga kura anaweza kuhakiki taarifa zake kwa njia zifuatazo:-

1. Mpiga Kura mwenyewe kufika katika kituo alichojiandikisha na kuhakiki taarifa zake katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika kituo hicho. Mtu mmoja kwenye familia anaweza kukagua taarifa za familia nzima.
2. Mpiga Kura kupitia simu yake ya kiganjani kupiga namba *152*00# na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
3. Mpiga kura kupiga simu namba 0800112100 na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
4. Mpiga Kura kuhakiki taarifa zake kupitia Tovuti ya Tume, www.nec.go.tz kwa kubonyeza sehemu iliyoandikwa 'uhakiki' na kuendelea kufuata maelekezo.

**Mambo ya kuzingatia.**

1. Daftari la awali la wapiga kura litabandikwa katika vituo vyote vilivyotumika kuandikisha wapiga kura.
2. Iwapo mpiga Kura amehakiki taarifa zake kwa kutumia njia yoyote kati ya hizo nne na kutaka kufanya marekebisho ya taarifa zake atatakiwa kwenda katika Ofisiza Halmashauri husika na kufanya marekebisho hayo.
3. Mpiga Kura anayehitaji kumuwekea pingamizi Mpiga Kura asiye na sifa zakuwemo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura ataenda katika Kituo kilicho pangwa kwenye Halmashauri husika.
4. Wapiga kura wanatakiwa kutoa taarifa za ndugu waliofariki dunia ili waondolewe kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
5. Katika zoezi hili hakutakuwa na Uandikishaji wa Wapiga Kura Wapya. Aidha, hakutakuwa na Uboreshaji wa Taarifa za Wapiga Kura waliohama maeneo yao ya kiuchaguzi, waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika.

**Muhimu:** Kumbuka kuzingatia Kanuni za Afya kwa kufuata Maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya Virusi vya Corona

**Dkt. Wilson Mahera Charles**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

**Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar Es Salaam, Tel.+255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.**

215775002

# NCCR-Mageuzi yafungua milango

**Na Elizabeth Zaya**

NCCR-Mageuzi imetoa ratiba yake rasmi ya uchukuaji na urejeshaji wa fomu ya kwa watia nia ya udiwani, ubunge, uwakilishi na urais kuanzia Juni 15 hadi Julai 8, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Elizabeth Mhagama, alisema Katiba ya chama hicho inaeleza wazi namna ya chama hicho kushirikiana na vyama vingine.

"Sisi hatuna tatizo lolote katika kushirikiana na vyama, hatuwezi kukataa na Katiba yetu inaeleza na imeweka wazi namna tunavyopaswa kushirikiana," alisema Mhagama.

Alisema tayari fomu kwa ajili ya wagombea wa nafasi hizo zimesambazwa mikoa yote na kwamba fomu za udiwani zitachukuliwa katika ofisi za kata za chama hicho, ubunge, katika ofisi za makatibu wa majimbo na kwamba za uwakilishi zitachukuliwa Zanzibar.

Kwa upande wa nafasi za watia nia ya urais, alisema fomu hizo zitachukuliwa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa chama hicho makao makuu.

"Kiongozi katika nafasi yoyote tunayemtaka lazima awe na sifa za kiongozi zilizoainishwa kwenye Katiba ya chama chetu. Tunataka awe na maadili ya Kitanzania na ajipime kama ana maadili na kusimamia maslahi ya wote, awe imara, shupavu na kusimamia maslahi ya Watanzania wote bila ubaguzi wala upendeleo," alisema Mhagama.

"Tunaamini tunao wanachama wenye sifa ya kutetea katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao watakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi magumu kwa maslahi ya taifa letu kwa kuwawajibisha viongozi wasiotekeleza majukumu yao."

Mhagama alisema vikao vya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama hicho vya kupendekeza wagombea katika nafasi mbalimbali vitaanza kuanzia Julai 8, 9 hadi 10.

Aliwaomba wagombea wa nafasi ya urais kujitokeza kuchukua fomu na kuanza kuzungumza kwa ajili ya kutafuta wadhamini.

# Tanga yatajwa kinara matukio ukatili wa watoto

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema vitendo vya ukatili kwa watoto kwa kipindi cha miaka miwili vimeongezeka huku Mkoa wa Tanga ukitajwa kuwa kinara wa matukio ya ukatili.

Kwa mujibu wa Takwimu za Jeshi la Polisi kwa miaka miwili mfululizo 2018 hadi 2019, ongezeko la matukio 1,189, huku matukio ya ubakaji, mimba kwa wanafunzi na ulawiti yakiongoza.

Kufuatia hali hiyo, Waziri Ummy ameagiza kufanyika kwa utafiti wa kina kujua sababu za mikoa kujirudia kwenye matukio ya ukatili.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika inayoadhimishwa leo.

Alisema vitendo vya ukatili vinaendelea kuongezeka, ambapo kwa mwaka 2018 jumla ya matukio 14,491 ya ukatili dhidi ya watoto yaliripotiwa, ikilinganishwa na matukio 15,680 yaliyoripotiwa mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la matukio 1,189.

Vile vile, alisema kwa mwaka 2018 aina ya matukio yaliyoongoza ni ubakaji (matukio 5,557), mimba za mwanafunzi (matukio 2,692) na ulawiti (matukio 1,159).

"Kwa mwaka 2019, matukio yaliyoongoza ni ubakaji (matukio 6,506), mimba za wanafunzi (2,830) na ulawiti (1,405)," alisema.

Hata hivyo, alisema mikoa ya kipolisi iliyoongoza kuwa na matukio mengi zaidi ya ukatili dhidi ya watoto kwa mwaka 2018 ni Tanga (1,039), Mbeya (1,001), Mwanza (809) na Arusha (792).

"Pia kwa mwaka 2019 ni Mkoa wa Tanga (matukio 1,156), Mkoa wa Kipolisi-Temeke (844), Mbeya (791) na Mwanza (758)," alisema.

Alisema pamoja na mifumo mizuri ambayo serikali imeweka ili kusimamia na kulinda haki za watoto, bado watoto wanaendelea kufanyiwa.

"Serikali inaendelea kuchukua hatua kukabiliana na vitendo vya ukatili, pia wazazi hakikisheni mnafuatilia mienendo ya watoto wenu na kuimarisha ulinzi wa watoto," alisema.

Kadhalika, alisema kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kwa mikoa inayoongoza kwa matukio hayo ili kujua sababu halisi zinazochangia na kusaidia serikali kuchukua hatua zaidi.

Waziri Ummy alisema serikali imeendelea kutoa huduma za ustawi wa jamii katika mahabusu tano za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam.

"Katika mwaka 2019/20, watoto 138 waliwezeshwa kupata huduma hizi ikilinganishwa na watoto 354 mwaka 2018/19, serikali imeanzisha mahakama maalumu za kusikiliza mashauri ya watoto ambazo zimeongezeka kutoka mahakama tatu mwaka 2015/2016 hadi kufikia mahakama 141 mwezi Machi, 2020 nchi nzima," alisema.

Alisema serikali inafanya mapitio katika baadhi ya vipengele vya Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 pamoja na kanuni zake ili kukidhi mahitaji ya sasa katika utoaji wa haki na ulinzi kwa ajili ya ustawi wa mtoto nchini.

Aliwataka wazazi kuhakikisha wanakaa nyumbani kwa muda mrefu ili kuendelea kuimarisha huduma za uchangamshi wa watoto.

Aliwaomba wanahabari, kuendelea kufichua vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hasa vitendo vya ubakaji, ulawiti na mimba za utotoni kutokana na kuongoza katika jamii kwa sasa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Watoto wa Wizara hiyo, Sebastian Kitiku, alisema sababu zinazochangia mikoa kuwa kinara wa matukio ya ukatili ikiwamo Tanga ni mila na desturi.

Alisema pia mkoa huo utaratibu wa wazazi kuruhusu watoto kwenda ufukweni na kusherehekea sikukuu inachangia matukio hayo.



Ofisa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori (kushoto), akimpongeza Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali, Charles Mbuge (katikati), kwa kupandishwa cheo kuwa Mkuu wa JKT, wakati wafanyakazi wa benki hiyo walipotembelea Makao Makuu ya Jeshi hilo wilayani Chamwino, mkoani Dodoma. Kulia ni Meneja Uhusiano na Serikali wa Benki ya NMB, Josephine Kulwa na Meneja wa Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# CUF yaikataa Chadema, ACT ushirikiano

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimesema kuwa hakitashirikiana na vyama vya Chadema na ACT-Wazalendo katika uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi wa Cuf Taifa, Juma Kilaghai, alisema chama hicho hakiwezi kushirikiana na vyama hivyo kwa sababu wamejifunza kwa kilichotokea katika uchaguzi wa mwaka 2015.

Mwaka 2015 vyama vya upinzani viliungana na kuunda umoja wa Katiba ya Wamanchi (Ukawa), ulianza wakati wa mchakato wa katiba mpya mwaka 2014, na kwenda hadi wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu ambao waliingia makubaliano ya kusimamisha mgombea mmoja kwenye nafasi mbalimbali.

"Kwa kilichotokea katika uchaguzi wa mwaka 2015 kilitufundisha, hatuwezi kurudia kosa, sisi tuko tayari kushirikiana na vyama vyenye nia ya dhati na kile wanachokizungumza," alisema Kilaghai na kuongeza:

"Tulishirikiana na Chadema kwa sababu walisema kwamba wanapambana na rushwa, lakini cha kushangaza walitoka nje ya kile wanachokizungumza na kukaribisha wala rushwa kugombea nafasi za juu ndani ya chama chao, na sababu hiyo ndiyo ilichangia CUF kuvurugana na kina Maalim Seif ambao sasa hivi wako ACT-Wazalendo na wanashirikiana tena."

Alisema ratiba ya uchukuaji na urejeshaji wa fomu kwa watia nia kwa nafasi ya urais mwisho ni leo na kwamba mpaka juzi walikuwa na mtia nia mmoja tu kwa nafasi hiyo, Mutayesa Yemba.

Kwa watia nia kwa nafasi ya udiwani, uwakilishi na ubunge alisema wanatarajia kufunga ratiba hiyo Julai 27 na 28 kuanza vikao kwa ajili ya uteuzi wa wagombea.

Alisema mpaka sasa idadi ya watia nia kwa nafasi za udiwani, ubunge na uwakilishi ni kubwa.

# TANGAZO

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

## SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

Siku ya mtoto wa Afrika imekuwa ikisheherekewa kila tarehe 16 mwezi Juni ya kila mwaka tangu mwaka 1991 ambapo ilianziwshwa na umoja wan nchi za Kiafrika wa kipindi hicho (OAU). Siku hiyo inalengea kuwakumbuka walioshiriki katika maandamano ya Soweto ya mwaka 1976 katika tarehe hiyo ya 16 Juni. Siku hii inalenga pia kuendelea kutoa elimu kwa jamii kwa ajili ya kuboresha masuala ya haki ya elimu kwa watoto.

Siku hiyo katika mji wa Soweto Afrika Kusini, zaidi ya watoto wenye asili ya afrika 10,000 waliandamana kupinga ubovu wa elimu inayotolewa na kudai haki yao ya kufundishwa kwa lugha yao wanayoifahamu. Mamia ya wanafunzi walipigwa risasi mmojawapo akiwa mtoto maarufu Hector Peterson. Zaidi ya watu mia waliuawa katika maandamano hayo ndani ya wiki mbili na zaidi ya maelfu ya watu walijeruhiwa.

Siku hii pia inalenga kutoa elimu kulingana na hali ya haki za watoto Afrika na kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Afrika wa haki na ustawi wa mtoto wa mwaka 1990 kwenye vipengele vya II hadi vya XXII.

Matatizo wanayopitia watoto mara nyingi yanachangia ukuaji wao kuwa watu wazima, hivyo tusipohakikisha kuheshimu na kulinda nafasi ya mtoto katika jamii zetu hasa katika elimu, afya, lishe na ulinzi wa mtoto, hatutaweza kuendeleza jamii na uchumi wetu ipasavyo. Kuwekeza katika watoto sio tu kitu bora zaidi kufanya kwa ustawi wao na maisha bora bali ni muhimu kwa kujenga zaidi jamii yenye ukuaji wa kiuchumi na ujenzi wa taifa kwa ujumla.

Mwaka huu haki za watoto zimekuwa mashakani kutokana na janga la Corona lililopelekea haki nyingi za watoto kuvunjwa ikiwemo ulinzi dhidi ya ukatili, haki ya elimu, ajira kwa watoto, haki ya afya na haki nyingine nyingi ambapo imepekleea watot wengi kuoata mimba za utotoni, kuozeshwa pamoja na kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali.

Taarifa ya haki za binadamu ya mwaka 2019 inayotolewa na kituo cha sheria na haki za binadamu ambayo ilizinduliwa tarehe 29 April imeonesha kuwa watoto bado hawako salama na kunahitajika nguvu ya ziada kuendelea kuhakikisha ulinzi wao. Taarifa hiyo imeorodhesha mambo kadhaa ambayo bado yamekuwa kikwazo kwa haki za watoto nchini Tanzania;

**Elimu**
Haki ya elimu hasa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao asilimia kubwa ni watoto wenye umri chini ya miaka 18, imekumbwa na changamoto nyingi kama ifuatavyo;

i. **Ukosefu wa mashimo ya vyoo, madarasa na mabweni**
Shule nyingi zina upungufu wa vyoo, madarasa na mabweni kitu kinachoathiri upatikanaji wa elimu kwa watoto . Ripoti ya mkaguzi mkuu wa serikali inasema kuwa kuna upungufu wa asilimia 88% na upungufu huu unathiri upatikanaji wa elimu na inachangia sana watoto kuacha shule.

ii. **Upungufu wa walimu na nyumba za walimu**
Hii imekuwa changamoto inayoendelea kudidimiza haki ya elimu kwa watoto nchini Tanzania. Katika mwaka 2019 serikali iliripoti kuwa zaidi ya walimu 80,000 wanahitajika katika shule za Sekondari na Msingi.

iii. **Umbali mrefu kwenda na kutoka shuleni**
Hii ni changamoto kubwa hasa kwa watoto walioko vijijini ambako hakuna njia nyingine za usafiri na ambapo hawajiwezi kiuchumi ambao hulazimika kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi kutoka shuleni. Kwa mfano katika wilaya ya Muheza Tanga watoto wanatembea hadi kilometer 30 kwenda shule na ni sababu zinazowafanya wengi kuacha shule, wasichana kupata ujauzito na kupitia vitendo vya ukatili njiani.


iv. **Hedhi salama shuleni**
Watoto wa shule wengi hawana elimu kuhusu masuala ya hedhi na hivyo kushindwa kujua cha kufanya pale inapotokea wameanza kuona siku zao za hedhi. Masuala ya hedhi yanaathiri sana watoto walioko shuleni kwani wengi huacha shule kipindi cha hedhi kuogopa aibu kutokana na kutokuwa na vifaa vya hedhi kama taulo za kike. 48% ya watoto wa kike hukosa shule sababu ya hedhi na 36% wanabaki nyumbani hiyo ni kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2018. Pia shule nyingi zinakosa sehemu za usiri na maji safi na salama kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike. Serikali ya Tanzania ilitangaza mwaka 2019 kurudisha kodi kwenye taulo za kike hali inayozidi kuwakandamiza watoto wa kike.

v. **Kuongezeka kwa walimu wanaobaka watoto wa kike na kuwapa ujauzito.**
Usalama wa watoto wakiwa mashuleni umekuwa ukihatarishwa zaidi na walimu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike na kuwasababishia ujauzito. Taarifa ya tume ya utumishi wa waalimu inasema kuwa walimu 162 wamesimamishwa kazi kutokana na sababu za kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi waka 2016. Mwaka 2018 hadi 2019 kituo cha sheria na haki za Binadamu kilipokea kesi 24 za walimu waliokuwa na mahusiano na wanafunzi.;

vi. **Kuongezeka kwa mimba za utotoni**
Mimba za utotoni zimeendelea kuwa sababu inayochangia kuwarudisha nyuma watoto kielimu na kijamii. Mwaka 2018 hadi 2019 kituo cha sheria na haki za Binadamu kilipokea taarifa ya zaidi ya kesi 2540 za mimba za utotoni. Hali hii imekuwa mbaya zaidi hasa kipindi hiki cha janga la Corona ambapo kwa miezi mitatu tu wasichana zaidi ya 100 wamepata ujauzito. Kulingana na tamko la raisi la kuzuia wasichana kurudi shule baada ya ujauzito,ndoto nyingi za wasichana hao zinazidi kupotea huku wakitumbukia kwenye wimbi la kuwa mama katika umri mdogo na kuendelea kudidimia katika umasikini

**Mauaji ya Watoto Njombe**
Mwaka 2019 kulitokea wimbi la mauaji ya watoto mkoani Njombe ambako kituo cha sheria na haki za binadamu kilifanya utafiti mdogo na kugundua kuwa watoto hao waliuawa kutokana na sababu za kishirikina.

**Kuongezeka kwa ukatili wa kingono kwa watoto.**
Taarifa za jeshi la Polisi Pamoja na utafiti wa mtandaoni wa Kituo cha sheria na haki za binadamu ilionesha kuwa ukatili wa kingono kwa watoto ikiwemo ubakaji na ulawiti unazidi kuongezeka. Mwaka 2019 Januari hadi Juni kesi 126 ziliongezeka kulinganisha na mwaka 2018 na ulawiti uliongezeka kwa kesi 141.




Kwa ujumla kuanzia mwaka 2016 hadi 2019 jeshi la Polisi limepokea kesi zaidi ya 42,824 na kuna kesi nyingi ambazo haziripotiwi na hivyo taarifa zake kupotea. Katika utafiti wa mtandaoni uliofanywa na kituo cha sheria na haki za Binadamu 84% ya kesi zilizopokelewa ni ukatili wa kingono wa watoto.

**Ukatili wa kimwili**
Hii imekuwa changamoto kubwa pia kwa watoto nchini Tanzania kwani wamekuwa wakipitia ukatili wa kimwili hasa sehemu za shuleni ikiwemo adhabu kali na sehemu za nyumbani. Ukatili mwingi wa kimwili umekuwa ukeketaji hasa mikoa ya Mara, Dodoma na Singida, vipigo, na mauaji ya Watoto hasa huko Njombe. Kumekuwa pia na adhabu zisizofaa kwa watoto ikiwemo kuchomwa mikono na adhabu nyingine. Watoto pia wamekuwa wakiingizwa katika migogoro ya wazazi wao hadi wengine kuamua kuwaua au kuwapa adhabu kali. Watoto 26 waliripotiwa kufa kutokana na ukatili wa kimwili kwa mwezi Januari had Disemba 2019.

**Ndoa za utotoni**
Watoto bado wanaathiriwa na ndoa za utotoni japokuwa mahakama ya rufaa mwaka 2019 ilitoa amri kwa serikali kubadilisha Sheria ya ndoa lakini hali hiyo bado imekuwa changamoto kwa watoto kuendelea kuolewa katika umri mdogo. Kipindi cha Corona kesi nyingi za ndoa za utotoni zimeendelea kuripotiwa katika vyombo vya Habari.

**Maambukizi ya virusi vya UKIMWI Kwa Watoto**
Kutokana na watoto wengi kufanyia vitendo vya ukatili wa kingono , hali hiyo imezidi kuwaweka katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Taarifa ya UKIMWI ya mwaka 2017 nchini Tanzania inaonesha kuwa kundi la miaka 15 hadi 24 liko katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

**Ajira kwa watoto**
Hali hii imeendelea kuwanyanyasa watoto. Sheria ya ajira na mahusiano kazini inaruhusu ajira kwa watoto kuanzia miaka 14 lakini ajira hizo zinaathiri ustawi wao ikiwemo elimu. Nchini Tanzania kuna watoto zaidi ya 15 milioni na Watoto milion 4.2 ambao ni asilimia 28. 8 wanafanyishwa kazi kulingana na taarifa ya mwaka 2016 ya serikali ikishirikiana na Shirika la kazi duniani. Kazi hizo nyingi ni kazi za ndani, migodini na mashambani. Ajira kwa watoto inaathiri zaidi ukuaji pamoja na ustawi wao kwani wengi wanafanyishwa kazi ambazo haziendani na umri wao na saa nyingine kusababisha wasiweze kuendelea na shule.

**Watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani**
Hawa watoto wamekuwa katika athari zaidi ya kufanyiwa vitendo vya ukatili, ajira, na kutumika katika biashara za ngono. Wanaishi mitaani bila uangalizi wowote na mara nyingi hawahudhurii shule. Tanzania kuna zaidi ya watoto 6,393 wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

**Watoto walio na migogoro na sheria**
Kumekuwa na changamoto mbalimbali kwa watoto wengi wanaofanya makosa ya jinai hivyo kukamatwa na kuhukumiwa vifungo. Kumekuwa hakuna huduma sahihi kwa watoto hasa polisi, magereza na hata mahakamani kwani watoto wamekuwa wakikosa huduma hasa ya uelewa kuhusu masuala ya haki na kutendewa kwa upendo kama mtoto.

**NINI KIFANYIKE**

i. Serikali iongeze bajeti ya utekelezaji wa mpango wa taifa wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto na wadau wanaohusika washirikishwe.
ii. Kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mtoto katika ngazi zote
iii. Serikali ya Tanzania irekebishe sheria ya ndoa kama ilivyoamriwa na Mahakama
iv. Serikali itunge na ibadilishe sheria na sera mbalimbali kuruhusu watoto wanaopata ujauzito wakiwa shuleni kuweza kurudi shule
v. Vyombo vya usalama vitoe huduma rafiki kwa watoto wanaokinzana na sheria
vi. Watoto wapewe haki ya elimu na jamii ziache mara moja kutumikisha watoto wadogo na hasa katika ajira zinazowadhuru na zisizofaa
vii. Serikali na wadau waelimishe na kuhimiza jamii kuheshimu sheria na sera zilizowekwa ili kuwalinda watoto
viii. Vyombo vya usalama vihakikishe haki inapatikana kwa watoto waliofanyiwa ukatili
ix. Jamii itoe taarifa kuhusu watu wanaofanya ukatili kwa watoto
x. Wadau na mashirika mbalimbali waendelee kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda watoto
xi. Wizara ya elimu, sayansi na teknolojia kuhakikisha wanaweka mbinu na misingi bora kuwalinda watoto mashuleni dhidi ya walimu wanaowafanyia ukatili.
xii. Wizara ya elimu sayansi na teknolojia kuhakikisha wanazingatia utoaji wa elimu jumuishi bila kumbagua mtoto yeyote.

215774302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mtoto alindwe dhidi ya ukatili

**JUNI** 16, kila mwaka ni maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, lengo likiwa ni kupaza sauti na kuonyesha umuhimu wa mtoto katika maendeleo endelevu ya taifa lolote.

Siku ya Mtoto wa Afrika huadhimishwa kimataifa kote duniani kwa lengo la kutambua thamani, utu na umuhimu wa mtoto duniani, na siku hiyo ilitangazwa kuwa siku rasmi mwaka 1991 na Jumuiya ya Umoja wa Afrika.

Tanzania mwaka huu, inaadhimisha siku hii chini ya kaulimbiu ya "mifumo rafiki ya upatikanaji wa haki za watoto: Msingi imara wa kulinda haki zao".

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef), Tanzania ina watoto milioni 23, na kwamba bado kuna changamoto za udumavu, huku takwimu zikionyesha asilimia 32 ya watoto nchini wana udumavu, hiyo ikiwa ni sawa na watoto milioni tatu ambao wako chini ya umri wa miaka mitano.

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa), kimejikita katika kupaza sauti ya mwanamke na mtoto kupitia vyombo vya habari kwa takribani miaka 30, lengo likiwa ni kuhakikisha kuna jamii yenye usawa na isiyokuwa na matukio ya ukatili dhidi ya kundi lolote.

Tamwa inasema tatizo la udumavu linapaswa kushughulikiwa na wadau wote kwa sababu madhara ya udumavu ni makubwa ambayo athari zake zinaanzia ndani ya familia na baadaye taifa linaathirika pia.

Chama hicho cha wanataaluma kinabainisha changamoto zinazokawabili watoto kuwa ni ukatili wa kingono, kubakwa, kuingiliwa kinyume cha maumbile, kukeketwa, kupigwa na kuumizwa au kuuliwa, kulazimishwa kuolewa, kupata mimba, magonjwa na ulemavu utokanao na vitendo vya ukatili wa kingono.

Matukio ya watoto kulawitiwa ndani na nje ya familia yanaongezeka na zaidi watoto wa kiume wamekuwa katika hatari zaidi, huku watoto wa kike wakibakwa na kuharibiwa ikiwamo kuambukizwa maradhi mbalimbali.

Mbaya zaidi baadhi ya wanafamilia huyamaliza nje ya mahakama kwa kutoza faini za kimila na kumaliza kesi nyumbani, ili kuficha familia hasa inapotokea aliyehusika ni ndugu wa familia husika, ambaye analindwa huku aliyetendewa ukatili huo akibaki na jeraha maisha yake yote.

Kwa mtoto wa kiume aliyelawitiwa moja kwa moja huwa shoga anapokuwa mtu mzima, na ataendelea kufanyiwa hivyo na wakati mwingine kushinikiza kuendeleza kufanyiwa hivyo kwa nguvu na ndiyo mwisho wa maisha yake ya kuitwa baba wa familia.

Kwa mtoto wa kike huathirika kisaikolojia kiasi cha kutotaka kuwa na mahusiano, kujenga chuki na jinsia ya kiume, kutokuzaa kwa maana ya kukataa kuolewa na wakati mwingine kuwa mtoto mwenye roho ya tofauti kwenye jamii.

Kutokana na hali hiyo watoto huumizwa kisaikolojia dhidi ya vitendo hivyo na hakuna jitihada mahususi za kutibu saikolojia na hivyo kuishi na tatizo hili maisha yao huku utumikishwaji wa watoto nao ukiendelea katika maeneo mbalimbali hasa mashambani, migodini na mijini wanaonekana katika biashara za barabarani na kuombaomba.

Bahati mbaya sana wazazi na walezi wengi wameacha wajibu wao wa msingi wa malezi ya watoto kwa wasaidizi wa nyumbani ambao wamejichukulia jukumu la malezi ya watoto.

Watoto wamekuwa waathirika wakubwa wa teknolojia kwa picha zao kusambazwa ovyo bila kujali haki zao, picha nyingine za kuwadhalilisha na kutolinda utu watoto.

Changamoto nyingine imeletwa na janga la corona kwa kipindi hiki ambacho wanafunzi wako nyumbani bado kumeripotiwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto ikiwamo mimba za utotoni kwa mikoa ya Mtwara na Manyara.

Ni wajibu wa wazazi na walezi kuhakikisha usalama wa watoto nyakati wote, kuwa karibu nao na kuzungumza kwa uwazi mambo mbalimbali.

Kwa sasa utapeli na wizi wa kutumia watoto unaongezeka, mathalani jana mwanafunzi wa Shule ya Keland jijini Dar es Salaam kaibwa na dereva pikipiki ambaye alikwenda kumweka rehani eneo la Madale na kuchukua mtungi wa gesi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Maadhimisho ya Soweto yakumbushe kujali elimu

Na Adam Fungamwango

ELIMU kwa mtoto ni miongoni mwa mada kuu ambazo hutawala mataifa mbalimbali Afrika ikiwamo Tanzania, hasa wakati huu wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, ambayo hufanyika kila mwaka Juni 16.

Hapa nchini, jitihada mbalimbali zimefanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa elimu kuhakikisha kila mtoto awe wa maskini au tajiri wanapata elimu, ikiwamo rasmi na isiyo rasmi.

Wapo baadhi ya yatima na wengine kutoka katika familia maskini, ambao hupewa sare na vifaa vingine vya shule, lengo likiwa ni kuhakikisha kila mtoto anapata elimu.

Kimsingi siku hii inahimiza kupinga vitendo vyote vya ukatili kwa mtoto, lakini elimu nayo haiachwi nyuma, ndiyo maana mada kuu katika maadhimisho huwa inajikita kwenye elimu kwa mtoto bila ubaguzi wa jinsia.

Hivyo, siku hii inapoadhimishwa, ipo haja pia ya kuwasaidia watoto wa mitaani wenye umri wa kwenda shule, ambao wamekuwa wakizagaa wakiomba fedha badala ya kusoma.

Kundi hili nalo lina haki ya kupata elimu na bahati nzuri serikali imefuta ada kwa shule za msingi hadi kidato cha nne, hivyo ni vyema ukaandaliwa mkakati maalum wa kuwezesha watoto wa mitaani nao wapate elimu.

Hivyo, wakati huu wa kuwakumbuka na kutambua mchango wa watoto waliopoteza maisha katika mauaji ya Soweto, iwe pia ni wakati wa kuhakikisha mtoto anapata haki zake za msingi ikiwamo elimu.

Kila mmoja akitambua hilo, matukio ya ukatili kwa watoto hususani vitendo vya ubakaji na ulawiti, mimba za utotoni, ndoa za utotoni na ukatili wa kimwili vitakoma ndani ya jamii.

Vitendo hivyo vikikoma, kuna uwezekano mkubwa wa kupungua kwa watoto wa mitaani ambao wamekuwa wakidhurura kuomba fedha, huku wenzao wakienda shule kupata elimu.

Nikirejea kwenye maandamano ya wanafunzi wa Afrika Kusini, historia inaonyesha kuwa Juni 16 mwaka 1976 alfajiri, wakiwa na walimu wao, walikutana mtaa wa Soweto ili kuandamana kwa amani.

Wanafunzi hao kutoka shule mbalimbali walifanya maandamano makubwa kupinga utekelezwaji wa matumizi ya lugha ya kibantu (Kiafrikaans) kama lugha ya ufundishaji katika shule.

Walipinga matumizi ya lugha hiyo kama lugha ya ufundishaji, ambayo ililenga kutekeleza sheria iliyoitwa 'Afrikanaans Medium Decree ya mwaka 1974 '

Kwa kuzingatia sheria hiyo Kiingereza kilitakiwa kutumika katika masomo ya sayansi jumuishi na masomo ya mazoezi kwa vitendo, huku lugha za asili zikitumika kufundishia masomo ya dini, muziki na utamaduni.

Waliamua kuandamana kupinga ubaguzi wa rangi katika lugha za kufundishia baina ya watu weusi na wazungu, na waliamini mfumo huo ungewadumaza na kuwaandaa kufanya kazi za vibarua na si vinginevyo.

Polisi nao kwa upande wao walikuwa na kazi moja tu ya kuua, kwani walibeba silaha nyingi za moto na kuzielekeza kwa waandamanaji, hali iliyosababisha kuongezeka kwa idadi ya vifo.

Hivyo wakati leo ni maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, ni muhimu jamii kutafakari zaidi na kuvitafutia ufumbuzi vikwazo ambavyo vimekuwa vikisababisha mtoto na hasa wa kike kukosa elimu.

Ninasema hivyo, kwa sababu katika karne hii ya sayansi na teknolojia, kuna jamii ambazo bado zinamuona mtoto wa kike kama mtu wa kuolewa tu, hatakiwi kupata elimu, jambo ambalo si kweli.

Katika mazingira hayo, mtoto wa kiume amekuwa akipewa nafasi kubwa ya kusoma kana kwamba ndiye mwenye haki hiyo tu, na kumbe ni kukumbatia mila zilizopitwa na wakati.

Mila hizo zilizopitwa na wakati zinaendekezwa na baadhi ya makabila hasa yale yanayokeketa, ambayo mtoto wa kike akishafikisha umri wa kupevuka anakeketwa ikiwa ni maandalizi ya kuolewa.

Umefika wakati sasa maadhimisho haya ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo yalitangazwa rasmi mwaka 1991, yawe ni chachu ya kuibadili jamii kuacha ukatili kwa mtoto na vilevile apewe elimu.

Leo ni miaka 44 ya mauaji ya Soweto na pia ni miaka 29 tangu kuanza rasmi kwa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, hivyo kama ambavyo msisitizo umekuwa ni elimu kwa mtoto, basi jamii nayo ibadilike na kuondoa vikwazo vinavyosababisha akose elimu.

TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

# WARAKA Na. 1/2020

## MAAGIZO KWA MAWAKALA WA MELI KUHUSU MATUMIZI YA UTARATIBU WA "STORING ORDER" NA TOZO YA UCHELEWESHAJI MAKASHA

Kwa mujibu wa majukumu ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) chini ya Kifungu cha 12 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415, TASAC imetathmini changamoto zilizopo katika sekta ya uchukuzi kwa njia ya maji, ikiwa ni pamoja na zile zitokanazo na janga la COVID-19 katika nchi jirani, na kusababisha kuchelewesha upatikanaji wa makasha na nyaraka za usafirishaji.

Ili kukabiliana na changamoto hizo na kwa Mamlaka ya Shirika Chini ya Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Mawakala wa Meli wanaagizwa ifuatavyo:-

(a) Wasimamishe mara moja matumizi ya "Storing Order" katika kupokea makasha ili kuongeza ufanisi wa vyombo vya usafirishaji na huduma ya usafiri kwa ujumla na kupunguza gharama zisizokuwa za lazima.
(b) Wapokee makasha yote matupu ambayo hayajapokelewa kutokana na utaratibu wa "Storing Order".
(c) Madai yaliyopo ya "Demurrage Charges" yafanyike bila kutumia utaratibu wa "Storing Order"
(d) Waongeze muda wa "demurrage free period" katika kipindi hiki cha kukabiliana na janga la COVID-19 kwa makasha yaendayo nchi jirani kama inavyooneshwa katika Jedwali hapa chini

| Nchini | Muda Uliopo [Existing Free Period] | Muda Unaoelekezwa [Extended Free Period] |
|---|---|---|
| Rwanda (Kupitia Rusumo) | 30 | 55 |
| DRC (Kupitia Rusumo) | 55 | 80 |
| DRC (Kupitia Tunduma) | 55 | 65 |
| Zambia | 40 | 50 |

Muda unaoelekezwa utaanza kutumika kwa makasha yaliyoruhusiwa na mawakala kuanzia tarehe 15 Machi, 2020.

Shirika litafuatilia hali katika nchi jirani kabla ya kuelekeza kurejea kwenye muda uliopo sasa.

**Imetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**
**Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania**

**Jengo la PPF Tower, Sakafu ya 7 na 8, Kiwanja Na. 20/21, Mtaa wa Garden/Ohio,**
**S. L. P. 989, Dar es Salaam - Tanzania, Simu: +255 222 127 314, Nukushi: +255 222 127 313,**
**Barua Pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Tovuti: www.tasac.go.tz**

# Tamwa: Ukatili dhidi ya watoto wawaathiri kisaikolojia

**Na Mary Mshami, UDOM**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), kimesema kuwa matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto yanaongezeka kiasi cha kuwaathiri kisaikolojia.

Aidha, kimetaja matukio ambayo ni tatizo kubwa kuwa ni watoto wa kiume kuingiliwa kinyume na maumbile, ubakaji, utumikishwaji mashambani na migodini pamoja na ndoa za utotoni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Mwenyekiti wa Tamwa, Joyce Shebe, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, alitaja matukio mengine yaliyokikwazo kwa ustawi wa mtoto ni ukeketaji, vipigo na kuumizwa au kuuawa, vitendo vinavyowasababishia magonjwa na ulemavu.

Maadhimisho hayo yanafanyika chini ya kaulimbiu ya 'Mifumo rafiki ya upatikanaji haki za watoto: Msingi imara wa kulinda haki zao'.

"Wakati leo tukiadhimisha siki hii bado watoto wanakabiliwa na ukatili wa kuumizwa kisaikolojia dhidi ya vitendo hivi na hakuna jitihada mahususi za kutibu saikolojia ya watoto hawa, wanaishi na tatizo hili maisha yao yote," alisema na kuongeza:

"Utumikishwaji wa watoto nao ukiendelea katika maeneo mbalimbali hasa mashambani, migodini na mijini wanaonekana katika biashara za barabarani na kuombaomba."

Kadhalika, alisema takwimu zinaonyesha kwamba matukio mengi ya ukatili kwa watoto yanafanywa na watu wa karibu wa familia na nyumbani.

"Bahati mbaya wazazi na walezi wengi waumeacha wajibu wao wa msingi wa malezi ya watoto, wasaidizi wa nyumbani ndio wameachiwa jukumu la malezi ya watoto," alifafanua Shebe.

Alisema ukuaji na urahisi wa kutumia teknolojia umesababisha watoto kutumia mitandao kiholela kwa muda mrefu na kujifunza vitu vingi visivyoendana na maadili mema na makazi yamekuwa sehemu hatari kwa makuzi ya watoto.

Alisema, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 32 ya watoto nchini wana udumavu, hiyo ikiwa ni sawa na watoto milioni tatu ambao wako chini ya umri wa miaka mitano.

Aliwataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuhakikisha watoto wako salama na shule zitakapofunguliwa warejee shuleni wakiwa wenye afya njema ya mwili na akili.

"Janga hili la corona lisitumike kama njia au sababu ya kuwakatili watoto haki yao ya msingi ya kusoma. Hivi karibuni zimechapishwa habari kadhaa zinazoonyesha kuwa mimba za utotoni na matukio ya kuozesha watoto yameongezeka.

"Tamwa tunatoa wito kwa wazazi na walezi kuwa asiwepo mtoto ambaye hatorudi shule kwa sababu eti ameozeshwa au amefanyiwa ukatili uliosababisha maumivu ya kimwili au kiakili na mtoto kushindwa kwenda shule," alisema Shebe.

# Wabunge 55 Chadema wahojiwa

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imewahoji wabunge 55, kati ya 69 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kuhusu tuhuma za ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka ndani ya chama hicho.

Miongoni mwa waliohojiwa jana ni Devotha Minja, Yosepher Komba, Joyce Mukya, Jesca Kishoa, Dk. Immaculate Swale, Tunza Malapo, Suzana Mganukulima, Lucy Michael, Catherin Ruge na Haida Kenani pamoja na Cecil Mwambe.

Wengine walihojiwa wiki iliyopita ni Peter Lijualikali, Suzan Lyimo, Frank Mwakajoka, Lucy Mollel, Joseph Haule, Suzan Kiwanga, Paschal Haonga, Godbles Lema na Hawa Subira.

Risala Kabongo, Gimbi Masaba, Julius Kalanga, Antony Komu, Mary Muro, Rhoda Kunchela, Japhary Michael, David Silinde, Joseph Mbilinyi, Mchungaji Peter Msigwa, Esther Bulaya, Halima Mdee na Esther Matiko.

Mahojiano hayo yalianza Juni 11, mwaka huu ambapo walihojiwa wabunge 11 na Juni 12, walihojiwa wabunge wengine.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kumaliza kuhojiwa na Takukuru, Mbunge wa Ndanda (Chadema) Cecil Mwambe, alisema amejipanga kugombea ubunge katika jimbo lake la sasa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).




Mbunge wa Viti Maalum Chadema, Devotha Minja, akitoka nje ya ofisi za Makao Makuu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), jijini Dodoma jana, baada ya kuhojiwa kuhusu ubadhirifu wa fedha na matumizi mabaya ya madaraka katika chama hicho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugai atimua mbunge siku 7

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SPIKA wa Bunge Job Ndugai amemtimua bungeni kwa siku saba Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Salome Makamba, baada ya kudai kuwa azimio la marekebisho ya kanuni za Bunge limewasilishwa bila kuona rasimu yake.

Mbunge huyo ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kanuni za Bunge akichangia mjadala wa azimio hilo, alisema rasimu ya marekebisho hayo haikurudishwa kwa wajumbe na ameshtushwa na kuliona likiwasilishwa bungeni.

Kutokana na kauli hiyo, yalizuka majibizano kati yake na Spika Ndugai ambaye alimtaka aeleze mapendekezo yaliyoingizwa bila wajumbe wa kamati hiyo kushiriki.

Hata hivyo, mbunge huyo alisema mapendekezo hayo ni ya Spika, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, Naibu Spika ambaye ni Makamu Mwenyekiti na wajumbe wanaokubaliana na mapendekezo hayo, lakini sio yeye.

Kutokana na kauli hiyo, Spika alimtaka mbunge huyo kutoka nje kwani anachosema sio kweli na kwamba wabunge wa upinzani wameshirikishwa kwenye kila jambo.

"Nisikuone hapa mpaka baada ya siku saba, kama siku saba utanikuta mimi hapa sijui ni bangi sijui ni nini umeshiriki kila kitu tangu mwanzo sema kitu gani hukushirikishwa? Na posho zote umevuta," alisema.

Katika hatua nyingine, wabunge watatu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wamehama chama hicho na kuomba ridhaa ya kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wabunge hao ni Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Semesi Sware, Anna Kidarya na Latipha Chande.

# Tume yataka utungaji haraka sheria ya wazee

**Na Magdalena Haule, UDOM**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), imeishauri serikali kuharakisha utungaji wa sheria ya wazee, ili kuwezesha haki zao kulindwa.

Pia, imevitaka vyombo vya sheria kuendelea kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mikakati ya kukomesha mauaji ya wazee nchini.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti Tume hiyo, Mohamed Hamad, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wanapaswa kuendelea kuelimisha jamii kuhusu haki za wazee.

Kauli hiyo inakuja ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Kukuza Uelewa wa Dhuluma dhidi ya Wazee Duniani iliyofanyika jana kwa lengo la kuelimisha jamii suala la unyanyasaji wanaokumbana nao wazee.

Alisema kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inayosema 'Paza sauti dhidi ya wazee', huku ikitambua jitihada zinazofanywa na serikali na wadau dhidi ya wazee.

"Changamoto za wazee zinapaswa kutambuliwa na kufanyiwa ufumbuzi mapema, baadhi yake ni kutofaidika kwa mafao mbalimbali ya mifuko ya hifadhi ya jamii, huduma duni za afya, mauaji ya wazee, umaskini, kutelekezwa pamoja na manyanyaso yanayowakumba wazee," alisema.

# TRA yaita walipakodi kabla Juni 30

Na Gwamaka Alipipi

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewataka wafanyabiashara na walipakodi wote kuwahi kulipa kodi zao za awamu ya pili, pamoja na malimbikizo yote kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, aliyasema hayo alipokuwa anazungumza na walipakodi wa mkoa wa Lindi.

Aliwashauri walipakodi kutosubiri kulipa kodi zao tarehe ya mwisho ili kuepuka msongamano kitu ambacho kinaweza kusababisha usumbufu kwao na maofisa wa TRA.

"Lakini tunaomba walipakodi wetu wazingatie kuwa misongamano ni hatari hasa kwa kipindi hiki dunia inapopambana na janga la corona," alisema Kayombo.

Aidha, aliwakumbusha wamiliki wa majengo kulipa kodi zao mapema kuepuka adhabu ya kuchelewa kulipa na kusababisha usumbufu kwao.

Alisema kwa sasa viwango vya kodi ya majengo vimekuwa rafiki na kwamba kwa nyumba ya kawaida isiyo ya ghorofa ni Sh. 10,000 na ya ghorofa ni Sh. 50,000 kwa kila sakafu kwa nyumba zilizopo katika Jiji na miji na Sh. 20,000 kwa ghorofa lote kwa maeneo ya vijijini.

Aidha, aliwakumbusha wafanyabiashara kutoa risiti za mashine ya kielektroniki (EFD) kwa kuwa inasaidia katika utunzaji wa kumbukumbu za biashara na vile vile kuwa uthibitisho wa mwenendo wa biashara.

"Napenda kuwasisitiza wafanyabiashara wenye mauzo yanayozidi Sh. milioni 14 kwa mwaka watumie mashine na kutofanya hivyo wanatenda makosa," alisema Kayombo.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara ambao tayari wanazo mashine za EFD kuzitumia mashine hizo ipasavyo, kwa kutoa risiti kwa kila mauzo na risiti hizo ziwe na kiwango sahihi kilicho husika katika muamala huo.

Vilevile aliwakumbusha wananchi kudai risiti wanaponunua bidhaa yoyote na wahakikishe kiwango kilichoorodheshwa kwenye risiti kiwe sawa na kiwango cha pesa alichotoa.



Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Hashim Mgandulwa, akizungumza na baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo, mwishoni mwa wiki, alipofanya ziara ya kutembelea vijiji mbalimbali kushuhudia jinsi ufuta unavyokusanywa katika maghala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazee Kahama wakombolewa bima ya afya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imetenga Sh. milioni 31.9 kwa kipindi cha miaka mitatu na kuwakatia bima za afya iliyoboreshwa (CHF) wazee 7,990 wenye umri kuanzia miaka 60 na kuendelea.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa Baraza la Wazee la Halmashauri hiyo, Wilfred Birago, wakati akitoa taarifa ya Ofisi ya Mkurugenzi Anderson Msumba, anavyotatua kero ya matibabu kwa wazee katika kikao cha mwisho cha Baraza la Madiwani cha halmashauri hiyo.

Birago alisema, kila mwaka wa fedha, halmashauri inatenga Sh. milioni 10 kwa ajili ya kuwakatia bima za afya wazee wenye umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea na mwaka 2019/20 imetenga Sh. milioni 11.7 na kuwakatia bima wazee 3,320.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2017/18, halmashauri ilitenga Sh. milioni 10 na kuwakatia bima za afya wazee 2,150, huku wadau wa maendeleo wakiwakatia bima hizo wazee 270 kutoka kata 20 zinaunda halmashauri hiyo.

Pia Birago alisema kuwa, mwaka wa fedha 2018/19, halmashauri ilitenga Sh. milioni 10.2 na kuwakatia bima za afya wazee 2,250 lengo likiwa ni kuboresha na kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee.

"Tunamshukuru Mkurugenzi wetu Anderson Msumba kwa kuona umuhimu wetu na kututengea kiasi cha fedha kila mwaka na kutukatia bima za afya ya CHF, na kwa mwaka huu wa fedha 2019/20 tumetengewa kiasi cha Sh. milioni 11.7 na kuwakatia bima za afya wazee 3,380," alisema Birago.

Naye Katibu wa Baraza hilo, Anderson Lyimo, alisema kwa sasa malalamiko ya wazee yamepungua katika hospitali ya Kahama ikilinganishwa na kipindi cha nyuma baada ya ofisi ya mkurugenzi kutenga na kuwakatia bima za afya wazee kila mwaka.

Lyimo alimpongeza mkurugenzi kwa kutenga chumba cha wazee na daktari atakaye wahudumia wazee wakati wote na kuongeza imesaidia wazee kueleza matatizo yao, kutosimama kwenye foleni kwa muda mrefu na kupata dawa kwa wakati.

# Wito kuendelea kuchangia damu

**Na Mary Geofrey**

WATANZANIA wametakiwa kuendelea kujitolea kuchangia damu ili kuokoa maisha ya majeruhi na wanawake wanaojifungua ambao wana uhitaji mkubwa wa damu wakati wowote.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma Shirikishi za Tiba kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Dk. Lulu Sakafu, aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Duniani yaliyofanyika katika Hospitali ya Mloganzila, jijini Dar es Salaam.

Alisema mahitaji ya damu ni makubwa kwa majeruhi wa ajali, wanawake wanaojifungua, wagonjwa wa saratani na figo ukilinganisha na makundi mengine hali inayosababisha uhitaji kuendelea kuongezeka kulingana na idadi ya wagonjwa.

"Mahitaji ya damu ni makubwa Muhimbili ndio maana tukaiomba wizara, damu salama na kukubaliana tuwe na kitengo cha kukusanya damu pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kujitoa zaidi. Idadi ya wagonjwa inavyoongezeka ndivyo uhitaji unavyoongezeka," alisema Dk. Sakafu.

Dk. Sakafu pia alisema kuwa upungufu wa damu ni chupa 20 hadi 30 kwa siku katika Hospitali ya Muhimbili na kwamba katika Hospitali ya Mloganzila idadi ya wagonjwa wanaopokelewa ni waliopata ajali kwa sababu ipo jirani na barabara kuu ya Morogoro.

Naye Ofisa Mhamasishaji wa Damu kutoka Hospitali ya Taifa Muhmbili-Mloganzila, John Daniel, alisema mahitaji ya damu yanaendelea kuongezeka kwa kuwa wagonjwa wenye magonjwa ya muda mrefu na wanaolazwa wapo kila siku.

# Mafundi vyerehani waomba eneo ujenzi

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

UMOJA wa wajasiriamali wa ufundi vyerehani Kata ya Kagongwa wilayani Kahama mkoani Shinyanga, umeiomba serikali kuwapatia eneo ambalo watalitumia kujenga madarasa yatakayotumika kuwafundisha vijana ufundi wa kushona nguo ili kuimarisha uchumi wao.

Hayo yameelezwa na Mwenyekiti wa umoja huo, Manyasa John, baada ya kumalizika kwa ugawaji vitambulisho vya ujasiriamali kwa wanakikundi wa umoja huo vinavyotolewa na serikali kwa gharama ya Sh. 20,000 kila mwaka.

Alisema wanatamani kuwa wanatoa elimu kwa makundi ya vijana na wanawake ili nao wafahamu namna ya kushona nguo na kujipatia kipato, na kwamba wana mpango wa kufungua darasa ambalo ndilo watatumia kufundishia.

## HABARI BUNGENI



# Ma-Ras, wakurugenzi waagizwa usambazaji wa chanjo kwa wakati

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewaagiza makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuhakikisha usambazaji wa chanjo unafanyika kwa wakati.

Agizo hilo lilitolewa jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Taska Mbogo, ambaye alisema Katavi ni mkoa wa mwisho katika upatikanaji wa chanjo kwa mama na mtoto.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kinamama na watoto wa mkoa wa Katavi wanapata chanjo?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema pamoja na agizo hilo pia viongozi hao wahakikishe zinafika kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Ilisema lengo ni kuwakinga kinamama na watoto wachanga wote pamoja na mabinti wote wanaofikisha umri wa miaka 14 dhidi ya magonjwa mbalimbali yanayozuilika kwa chanjo.

Ilifafanua imekuwa ikinunua na kusambaza chanjo kwa ajili ya mikoa, halmashauri na vituo vyote hapa nchini kulingana na idadi ya walengwa katika maeneo husika.

Ilisema wizara imeendelea kusambaza chanjo katika Mkoa wa Katavi na mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa kinamama na watoto wanakingwa dhidi ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Ilisema serikali imekuwa ikinunua chanjo za Tetanus Toxoid (TT) kwa ajili ya kuwakinga mabinti wa umri wa kuzaa na wanawake wajawazito dhidi ya ugonjwa wa pepo punda.

Aidha, ilisema chanjo mbalimbali za kuwakinga watoto na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo zimekuwa zikinunuliwa, ikiwamo chanjo ya Pentavalent kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya donda koo, kifaduro, uti wa mgongo na homa ya ini kwa ajili ya kuzuia magonjwa ya nimonia na uti wa mgongo.

"Pia BCG dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu, bOPV na IPV dhidi ya ugonjwa wa kupooza, MR dhidi ya ugonjwa wa surua rubella, rota dhidi ya ugonjwa wa kuhara na HPV dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana wa umri wa miaka 14," ilisema.

Kadhalika, ilisema katika mwaka 2019, Mkoa wa Katavi ulitoa chanjo kwa watoto 38,468 na wajawazito 43,665 ikiwa ni kiwango cha asilimia 100 na hivyo kuzidi lengo la uchanjaji kimkoa.

"Utoaji wa huduma za chanjo ni kipaumbele cha kwanza cha Wizara ya Afya, serikali ya awamu ya tano ambapo kwa mwaka 2019/20 imetenga jumla ya Sh. bilioni 30 ili kuboresha upatikanaji wa chanjo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ukiwamo Mkoa wa Katavi," ilisema.

# Elimu uombaji mikopo yaanza



SERIKALI imesema imeanza kutoa elimu ya uombaji mikopo kwenye shule za sekondari, vyuo vya stashahada, kambi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Grace Tendega, na kuongeza kuwa ilianza kutekeleza mpango huo kuanzia Aprili hadi Juni mwaka jana.

Katika swali la mbunge huyo, alisema kumekuwa na changamoto kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kupata mikopo ya elimu ya juu.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto hizo?" Alihoji.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema ni lengo lake kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wahitaji na wenye sifa wanapata mikopo hivyo kutimiza ndoto zao za kupata elimu ya juu na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya taifa kikamilifu.

Ilisema imekuwa ikiongeza bajeti ya fedha za mikopo ambayo imeongeza idadi ya wanufaika kwa kiasi kikubwa.

"Kwa mfano, bajeti ya fedha za mikopo imeongezeka kutoka Sh. bilioni 348 mwaka 2014/15 hadi kufikia Sh. bilioni 450 mwaka 2019/20," ilisema.

Ilieleza kuwa idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka jumla ya wanafunzi 101,036 mwaka 2014/15 hadi wanafunzi 130,072 mwaka huu 2019/20.

Hata hivyo, ilisema pamoja na kuongeza bajeti, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeendelea kuimarisha utendaji ikiwamo kuboresha mifumo ya Tehama na kuendesha programu za elimu ya uombaji mikopo kwa usahihi kwa wanafunzi wa shule za sekondari ili kuongeza uelewa wao.

"Kwa mfano, kati ya mwezi Aprili hadi Juni, 2019, programu hizi ziliendeshwa katika shule mbalimbali nchini, na katika kambi zote 17 za JKT ambapo jumla ya wanafunzi 46,669 walifikiwa," ilisema.

Ilieleza kuwa lengo la jitihada zote hizo ni kuhakikisha wanafunzi wanafahamu sifa, vigezo na utaratibu wa kuwasilisha maombi ya mikopo kwa usahihi ili wale wote wenye sifa wapate mikopo na kutimiza ndoto zao za kupata elimu ya juu.




Habari na Augusta Njoji

# Mbunge ataka ukarabati mitambo skimu ya maji

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, ametaka serikali kutatua tatizo la uchakavu wa mitambo kwenye skimu ya maji ya Makonde kutokana na kushindwa kusambaza maji kwenye Mji wa Nanyamba.

Akiuliza swali bungeni jana, Chikota alisema skimu hiyo inakabiliwa na tatizo kubwa la uchakavu wa mitambo na umeme usio wa uhakika na hivyo kushindwa kusambaza maji hadi Mji wa Nanyamba.

Katika majibu ya Wizara ya Maji, ilisema eneo la Mamlaka ya Maji Makonde ina jumla ya watu 510,975 wenye mahitaji ya maji mita za ujazo 766,462 kwa mwezi.

Ilisema maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya maji yana wakazi wapatao 275,928.00 wenye mahitaji ya maji mita za ujazo 413,892 kwa mwezi sawa na asilimia 54 ya mahitaji ya wakazi wote wa Mamlaka ya Maji Makonde.



"Miundombinu iliyopo inaweza kuzalisha maji mita za ujazo 482,400 kwa mwezi kiasi ambacho kinakidhi mahitaji ya watu wote waliofikiwa na mtandao wa maji," ilisema.

Aidha, ilisema lengo la kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo, uwekezaji umepangwa kuelekezwa kwenye chanzo cha Mitema kwa kuwa chanzo hicho kina gharama za umeme nafuu zaidi katika uzalishaji maji.

"Uwezo wa chanzo hiki ni mkubwa kuliko vyanzo vingine na unaotosheleza mahitaji ya wakazi wote na kijiografia iko katikati ya eneo la Mamlaka ya Maji Makonde," ilisema.

Aidha, ilisema katika kuhakikisha wananchi wanaoishi maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji Makonde wanapata huduma ya maji, serikali kupitia Wizara ya Maji ikishirikiana na wadau wa maendeleo imetoa kipaumbele katika uboreshaji wa huduma ya maji katika mamlaka hiyo.

"Katika kipindi kilichoanzia mwaka 2015 hadi 2020, miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 13.436 imetekelezwa na miradi mingine inaendelea kujengwa.

Hata hivyo, ilisema serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni jitihada za kukabiliana na tatizo la uchakavu wa mitambo.

Pia ilisema itashughulikia miundombinu na umeme usio wa uhakika kwa kufanya marekebisho ya mitambo iliyopo pamoja na kutoa kipaumbele katika matumizi ya nishati jadilifu na hatimaye kupunguza gharama za uendeshaji kwa wananchi.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 16, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12
## YST yachoronga wanasayansi chipukizi kutumiwa kwenye gesi, nishati, kilimo



Ukurasa 14
**Mwalimu anavyowapa neno la kusimamia watoto wake**



Ukurasa 13
Umbumbumbu wa fikra unavyoangamiza watoto

## SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Inahamasisha uwekezaji, utambuzi, kutibu saratani kwa wenye ualbino

NA BEATRICE PHILEMON

WATOTO wenye ualbino ni miongoni mwa watu wanaopitia changamoto nyingi zikiwamo za kiafya, kunyanyapaliwa kwenye jamii na hata kuuliwa na viungo vyao kuuzwa ili kwa imani kuwa vikitumiwa huleta mafanikio.

Leo, tunapoadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika ni vyema kuwatambua wenye ualbino, ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu hali hiyo, kuwathamini na kuwasaidia zaidi.

Ualbino ni kukosa rangi ya asili au melanin kwenye ngozi, nywele na macho. Mwenye ualibino ni sawa na wengine kiutendaji bila kuangalia utofauti wa rangi licha ya kwamba ana uoni hafifu na ngozi inayoathiriwa haraka na mionzi ya jua.



Katibu Mkuu wa TAS, Mussa Kibimba (wa kwanza kushoto nyuma), Katibu wa TAS Tarime, Joseph Sinde (watatu nyuma kutoka kulia), wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa wa Ualbino, inayofanyika kila mwaka Juni 13. **PICHA: BEATRICE PHILLEMON.**

Akizungumza na Nipashe wakati wa Siku ya Kitaifa ya Kuongeza Uelewa wa Ualbino ambayo hufanyika Juni 13 kila mwaka, Ofisa Huduma, Chama cha Watu Wenye Ualbino (TAS), Christina Silas, anasema tunapoadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, kuna mitizamo mingi kuhusu wenye ualbino.

"Wapo wasiojali tofauti ya rangi lakini wengine wanawachukulia wenye ualbino kuwa ni tofauti tena hawafai kushirikishwa katika masuala mbalimbali ya kijamii," anasema Christina.

Katika kuadhimisha siku hii, anaipongeza serikali kwa kuhakikisha haki ya watoto wenye ualbino kupata elimu inazingatiwa tofauti na zamani.

"Sasa hivi idadi inayoandikishwa shule, imeongezeka kuanzia elimu ya awali na wanaendelea vizuri kama wengine wasio na ualibino tofauti na miaka ya nyuma, wazazi wengi walikuwa wakihofia kuwapeleka shule kuogopa mauaji na ukatili mwingine waliokuwa wakifanyiwa," Christina anaongeza

Akizungumzia elimu anasema, serikali inaendelea kujumuisha mahitaji ya wenye ualbino wanapokuwa shuleni mfano vifaa vya kujifunzia na kufundishia na TAS imeona hatua hizi baada ya kufanya utafiti mikoa ya kanda ya ziwa.

Mbali na hilo, kila mwaka serikali inaongeza walimu wa elimu maalumu ambao wanafundisha wanafunzi kulingana na ulemavu ambao huwasaidia wenye ualbino.

**KUTIBU SARATANI**

Christina anasema saratani ya ngozi ni tatizo kwa wenye ualbino na husababisha vifo kwenye umri mdogo, hivyo TAS, serikali na wadau wengine wamefanikisha kupata vifaa tiba vya saratani ya ngozi katika hospitali za rufani za Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Iringa, Singida, Mara na Unguja.

"Lengo ni kusaidia watoto na watu wazima wenye ualbino kupata ushauri, uchunguzi wa awali pamoja na tiba ya saratani mapema kwenye mikoa yao."

Pia, kuboresha takwimu na taarifa zote zinazohusu saratani ya ngozi kwa wenye ualbino.

Mwenyekiti wa TAS Wilaya ya Tarime, Joseph Sinde, anasema ingawa Tanzania inashiriki maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, umaskini vijijini unakwamisha wazazi kuwatunza watoto wenye ualbino.

"Umaskini unakwamisha wazazi na walezi kuwapeleka kwenye kliniki kuchunguzwa afya ya ngozi. Wengi wanaotoka vijiji vya mbali kufuata huduma za afya mijini. Kuna wanaotembea kilomita 50, au kulipa nauli ya kati ya Sh 5,000 hadi 10,000 kufikia kituo cha afya. Wengine wanashindwa matokeo yake wanakosa haki ya huduma za afya," anasema.

Hata hivyo, TAS Tarime inashindwa kuwafikia walio ya mbali ili kuwaelimisha kutunza watoto wenye ualibino, kuchunguza afya mapema, kufahamu saratani ya ngozi na kujikinga kwani hakuna vitendea kazi hasa usafiri na pesa.

Anawakumbusha kuwa kila baada ya miezi mitatu inakuwepo kliniki ya kuchunguza ngozi inayoendeshwa na Shirika la Standing Voice la Mwanza.

**WITO WA ELIMU**

"Sisi TAS Tarime tunatoa wito kwa serikali iendelee kutoa vipaumbele kwa watoto wenye ualbino kupata elimu ili wajimudu kimaisha kwa sababu asilimia kubwa ya wenye ulbino miaka ya nyuma walikuwa hawapati elimu na kupelekea wengi kuishi maisha ya kuombaomba na utegemezi. Yote yamesababisha unyanyapaa, ubaguzi na unyanyasaji dhidi ya wenye ualbino,"anasema Sinde.

Anaona kuwa wengi wakisoma na kuwa na elimu bora wataajirika au kujiajiri, watasaidia kuchangamana na jamii katika shughuli mbalimbali kama za kiuchumi na kisiasa.

**MATIBABU MUHIMU**

Sinde anataja changamoto ya upatikanaji wa mafuta kinga ya kuzuia mionzi ya jua kwa watoto wanaotoka kwenye kaya masikini kuwa ni hitaji la lazima kwa sasa.

"Upatikanaji wa mafuta haya ni shida sana ingawa tunapata kwa uchache kutoka serikalini na baadhi ya wadau wengine. Familia nyingi zilizo na watoto wenye ualbino haziwezi kununua vifaa vya kujikinga na mionzi ya jua kama vile miwani, kofia na mafuta," anasema

Mafuta kinga yanauzwa ghali na asilimia kubwa ya wazazi kwenye familia maskini hawawezi kumudu na hiyo inachangia kwa kiasi kikubwa watoto kupata kansa ya ngozi.

Katibu Mkuu wa TAS, Mussa Kabimba, akizungumzia uchunguzi na tiba ya saratani ya ngozi kwenye mikoa iliyopewa vifaa vya uchunguzi anasema, kufikia Juni 4 mwaka huu, wenye ualbino waliochunguzwa ni 1,501.

Kati ya hao 873 walikuwa wameungua na jua, 437 hawakuwa na tatizo, 235 walipatiwa tiba ya dalili za saratani ya ngozi na 68 walipewa rufaa kwa ajili ya msaada zaidi .

"Chama kinapenda kuufahamisha umma kuwa mauaji pamoja na vitendo vya kikatili vilivyokuwa vinawakabili wenye ualbino wakiwamo watoto havihusiani na masuala ya uchaguzi wa tiba. Hivyo wanaomba watu waache kupotosha jamii kwamba watu wenye ualbino wapo hatarini kwa sababu huu ni mwaka wa uchaguzi."

"Tunaishukuru serikali kwa kuendelea kulisimamia hili na mpaka sasa tunaona na kushuhudia watu wenye ualbino wanashirikishwa na kujumuishwa kwenye mambo mbalimbali hivyo kujenga uelewa na kuondoa imani potofu iliyokuwa inasababisha kundi hili kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo unyanyapaa," anasema

NA CRISPIN GERALD



Washiriki wa Sekondari Kisimiri wakielezea mradi walioubuni kusaidia Wamasai kuondokana na umasikini. **PICHA:YST.**

## SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# YST yachoronga wanasayansi chipukizi kutumiwa kwenye gesi, nishati, kilimo

KATIKA jitihada za kupata wanasayansi chipukizi watakaotoa majibu ya changamoto za Tanzania na Afrika, mbinu mbalimbali zinatumiwa kuwaatamia wasomi chipukizi watakafanikisha azma hiyo.

Wakati leo ni Maadhimisho ya Mtoto wa Afrika Tanzania ina mengi ya kujivunia katika kuwasaidia wanasayansi

kutoka mikoa yote ikiwa ni njia ya kuwaendeleza watoto kisayansi na teknolojia kuboresha maisha yao.

Watoto hawa wamepewa fursa ya kuandika wazo au ubunifu unaolenga kuibua mawazo mapya ya kimkakati na yanayotatua kero za kijamii.

Kuna maudhui ya teknolojia rahisi na za gharama nafuu, utafiti wa kutatua changamoto za jamii yanayoibua mbinu za kisayansi za kupunguza umaskini na maradhi.

Kuandaa mawazo hayo ili kupata wanasayansi chipukizi ni jukumu linalofanywa na Shirikisho la Wanasayansi Chipukizi (YST).

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR). Prof Yunus Mgaya, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya YST, anapongeza kazi ya kuhamasisha wanafunzi kupenda na kujifunza sayansi.

"YST imesaidia kuibua mawazo mbalimbali yanayotoa fursa ya kuleta suluhu kwenye changamoto zilizopo kwenye jamii zetu," anasema Profesa Mgaya.

Akizungumza Dar es Salaam, hivi karibuni anasema kuanzia January hadi Machi mwaka huu, shirikisho limekusanya mawazo 604 kutoka wanafunzi wa sekondari nchi nzima na baada ya kuyachuja yakapatikana mawazo 140 ya kisayansi.

Anaeleza kuwa ni matokeo ya hamasa inayotolewana YST kwa wanafunzi wa sekondari katika kuipenda na kuisoma sayansi ndiyo iliyoleta mwamko mkubwa wa kuipenda na kuisoma kwa vitendo.

> "Sote tunafahamu, serikali kwa sasa inahitaji wanasayansi wengi ili waweze kusukuma uchumi wa viwanda kwenda mbele na kufikia nchi ya uchumi wa kati, hivyo hizi harakati za YST zinalenga kuibua wataalam wa namna hiyo," anaeleza Dk. Kamugisha.

Prof Mgaya anaongeza kuwa, YST inaendesha program shule za sekondari ili kubadilisha mtazamo kwa wanafunzi na kwamba sayansi si ngumu ikiwaonyesha njia rahisi za kuielewa.

"Lakini pia, ikishirikiana na serikali, imewahamasisha wanafunzi kupenda sayansi kwa kuwafundisha mbinu za kufanya kwa vitendo mbali na nadharia ili isaidie kutatua changamoto zilizopo kwenye jamii yao," anasema.

**WALIMU WAFUNZWA**

Taasisi ya YST imetoa mafunzo kwa waalimu ya namna ya kufanya utafiti kisayansi na hadi sasa 176 pamoja na wanafunzi 2,416 kote nchini wamenufaika.

Anasema Young Scientists Tanzania ni jukwaa linalohimiza ubunifu barani Afrika, likilenga kuinua na kuboresha ujuzi wa sayansi kwa wanafunzi wa sekondari pamoja na kuhimiza kuipenda na kuifanya kwa vitendo ili kutoa matokeo chanya yatakayoleta suluhisho la changamoto za jamii, anaeleza Mgaya ambaye pia ni mwanasayansi mbobezi.

Aidha, YST inaandaa mashindano ya kila mwaka yanayowapa wanafunzi jukwaa maalum la kuonyesha tafiti za kisayansi wanazofanya wakiwa shuleni ambapo hupatikana washindi waliotengeneza utafiti unaotoa majibu ya tatizo la jamii.

**MUONGO WA MAFANIKIO**

Mwanzilishi mwenza wa YST Dk. Gozibert Kamugisha, anasema kwa miaka 10, wameshuhudia kuibua mawazo bora na ubunifu yaliyojikita kwenye fani ya sayansi yanayotoa suluhisho la matatizo ya jamii.

"Kwa namna ambavyo tumewahamasisha wanafunzi kupenda fani ya sayansi kwa kusoma masomo ya sayansi, ndivyo ambavyo tumekua tukipata mawazo mengi yanayoleta suluhu kwenye afya, mazingira, elimu, uchumi, kilimo na matatizo ya ukatili wa kijinsia, ambayo ni changamoto kwenye jamii ,"analifafanua Kamugisha.

"Ni mafanikio ya kipekee, ndani ya miaka 10 tumeweza kuijenga YST kama taasisi ya kitaifa na familia yetu ya wanasayansi imekua ikishiriki vyema kwenye maendeleo ya nchi yetu," anaongeza Dk. Kamugisha.

Program hiyo inayotekelezwa kwa kushirikiana na wadau wa kimataifa, ina lengo la kuchochea maendeleo endelevu kwa kuzalisha wanasayansi wengi na wenye ujuzi madhubuti, watakaoweza kuchochea maendeleo kwenye taifa hili.

"Sote tunafahamu, serikali kwa sasa inahitaji wanasayansi wengi ili waweze kusukuma uchumi wa viwanda kwenda mbele na kufikia nchi ya uchumi wa kati, hivyo hizi harakati za YST zinalenga kuibua wataalam wa namna hiyo," anaeleza Dk. Kamugisha.

Ukuaji na maendeleo ya YST katika kuhimiza maendeleo ya sayansi nchini yamefanikishwa kwa ufadhili wa wadau mbalimbali wa maendeleo ambao wanaonyesha nia ya kupatikana wataalam wa sekta ya mafuta, madini, teknolojia na nishati.

**KUIBORESHA AFRIKA**

Kwa mujibu wa meneja mradi wa YST, program ya kuhamasisha sayansi shuleni, inachangia kwenye mpango wa kitaifa wa miaka mitano kama ulivyochapishwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Program hii inaendana na mpango wa Umoja wa Afrika (AU), kupitia mpango mkakati wa kuinua elimu katika bara la Afrika. (CESA 2015-2025).

Lengo ni kuinua mfumo wa elimu ya Afrika na mafunzo katika kufanikisha dira ya kujenga Umoja wa Afrika kufikia mwaka 2063.

"Pia ni kufanikisha mpango huo kwa kuimarisha mtaala wa sayansi na hisabati kwa mafunzo ya vijana, pamoja na kutoa ujuzi wa kisayansi na utamaduni kwenye jamii," anasema Ofisa Maunganisho wa YST Titus Mteleka.

Mratibu wa YST Mkoa wa Mbeya, Beatus Mayunga, anasema sayansi ina umuhimu wa kipekee kwa maendeleo ya nchi. Shirikisho hili la wanasayansi linatoa fursa ya kipekee kwa wanafunzi kuwa bora kwenye fani ya sayansi.

Mayunga ambae pia ni mwalimu wa sayansi katika Sekondari ya Pandahill iliyopo mkoani Mbeya, anashauri serikali kuweka utaratibu maalum kwenye kila shule ya sekondari wa kuhamasisha wanafunzi kupenda sayansi pamoja na kuongeza uwekezaji wa vifaa, utaalamu na teknolojia shuleni ili kuhamasisha ukuaji wa fani hiyo.

Mayunga anabainisha kuwa mojawapo ya changamoto inayokwamisha maendeleo ya sayansi nchini ni uwapo wa nadharia kwa wanafunzi kwamba sayansi ni ngumu, jambo linalohitaji kufanyiwa kazi kubwa kwa kubadilisha mtazamo wa wanafunzi kuhusu sayansi, lakini pia pawapo na watu wa mfano kwenye jamii waliofanikiwa kwenye sayansi ili wawe mfano kwa wanafunzi.

YST linatoa nafasi kwa walimu na wanafunzi ya kuwa wakala wa mabadiliko nchini kwa kuhamasisha utafiti wa kisayansi.

Mtandao wa shirikisho wa kuwanoa wanafunzi unatoa mwanga kwa changamoto wanazokabiliana nazo kila siku. Pia inawapa wanafunzi ujasiri wa kufuatilia ndoto zao na kutangaza elimu asilia ya kisayansi na utamaduni," anaongeza Mayunga.



Washiriki kutoka Sekondari ya Mwakani wakielezea mradi wao wa ubunifu kwa washindi wa mashindano hayo ya kazi za kisayansi yaliyofanyika mwaka jana na kuratibiwa YST. **PICHA: YST.**

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

## SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Umbumbumbu wa fikra unavyoangamiza watoto



Watoto kuteswa, kuumizwa na kutolewa kafara ni taratibu ambazo huwaangamiza watoto katika jamii za Afrika. **PICHA: MTANDAO.**

WATOTO wa leo wamepitia matatizo mengi kuanzia kuozwa utotoni, kunyanyaswa kingono, waganga wa kienyeji kufanya biashara ya viungo vyao hasa wale ambao ni albino na wengine kufanywa kafara.

Leo yanapokumbukwa mauaji ya watoto waliokuwa wanasoma shule mbalimbali kwenye mji wa Soweto nchini Afrika Kusini, tunaiadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika.

Darubini ya Soweto iliyo msingi wa kumuenzi na kumthamini mto wa Tanzania pia inatukumbusha kuwa watoto zaidi ya 200 waliuawa na polisi kwa kuandamana na kupinga baadhi ya sera za kibaguzi zilizotaka wafundishwe kwa lugha za asili za Kiafrikana.

Huo ni ukatili uliofanywa na serikali ya kibaguzi dhidi ya watoto mwaka 1976, lakini hata leo kuna watu wanaowaua maelfu ya watoto hapa Tanzania kila mwaka.

Hawa ni wale walioamua kuusaka utajiri kwa nguvu za giza za kuwanyanyasa watoto badala ya kutumia nguvu na akili.

Watoto wanatumiwa kama chanzo cha kupata utajiri unaosakwa kwa nguvu na maelekezo ya waganga na watu wanaoamini katika ushirikina.

Mathalani, Masambu Nduguye ni mchimbaji mdogo wa madini, ambaye zamani alikuwa anachimba vito. Tunduru mkoani Ruvuma na Mirerani mkoa wa Manyara.

Mchimbaji wa madini, anasema kuna wakati migodini hasa kwenye machimbo ya vito, wafanyabiashara huwatumbukiza watoto mshimo na kuwalipua kwa baruti wakiamini kuwa mgodi utatema. Au madini yatapatikana kwa wingi.

Anasema matendo hayo ambayo ni kutumia nguvu za giza katika kutafuta utajiri husababisha watoto kutoweka kwani huchukuliwa kutoka mikoa ya mbali na kufikishwa kwenye sehemu zenye machimbo hayo.

Lakini, Nduguye anawauliza wanaowanyanyasa watoto hata kuwalipulia kwa baruti migodini na kuwazika, inakuwaje wanashindwa kujiuliza swali hili:

Kama utajiri ungekuwa unapatikana kwa wepesi hivyo si hata waganga na wanaopiga ramli wangeshatajirika mara moja na kuacha kazi za kutafuta pesa ikiwa ni pamoja na kuandika mabango kwenye miti kusaka wateja?

Anasema huu ni ushetani kwa sababu watoto wengi wametoweka na kupotea na hajulikani walipo kumbe walitiwa 'kitanzi' migodini kwenye machimbo ya vito kama tanzanite Mererani, rubi na dhahabu.

"Eti kafara hizo hufanya migodi icheue madini baada ya kuzindikiwa viungo vya albino, watoto, au ngozi zao."

Kwa mujibu wa asasi ya kuwajali na kuwatetea watu wanaoishi na ualbino ya Under the Same Sun (UTSS) , tangu mauaji ya alibino yalipoanza mwaka 2006 yameua watu 76 , kati yao walionusurika kutekwa ni 63 wakati makaburi 18 yalifukuliwa kusaka miili yao.

Katika manyanyaso hayo kuna watoto albino waliuawa na miili yao kutumiwa kishirikina kwamba ni chanzo cha utajiri, mafanikio kisiasa na bahati kwenye maisha ya jumla.

Kuna madai kuwa kwenye maduka na sehemu nyingine zinapofanyika biashara viungo vya watoto hawa vinakuwapo na hutumiwa na wajasiriamali au watu wanaotumia nguvu za giza badala ya akili kusaka utajiri.

Mauaji ya watoto hufanywa na baadhi ya wanaume wanaoamini kuwa kumbaka na kumnajisi mtoto wa kike kunaongeza nguvu na hamu ya kujamiiana hivyo wasichana wadogo wamekuwa waathirika wa matendo hayo hata kufariki dunia.

Hata, wanaume wengine wenye magonjwa na wengine wanaoamini kuwa wana mkosi na kukataliwa au kutofanikiwa kupata wenza huwabaka na kuwanajisi watoto wa kike kwa imani kuwa wataondoa nuksi na kufanikiwa kuwa na afya njema na kupata ndoa.

Collin Mlawa mwanafunzi katika Shule ya Msingi Goba jijini Dar es Salaam, anapozungumza na Nipashe kuhusu kuwanyanyasa watoto, anasema watoto wanakerwa na taarifa za mauaji au kupotea kwa wenzao kwa kutumia matunguli na ramli ambazo husababisha vifo na mateso kwa watoto na kwamba huko ni kufanya mambo nje ya mstari.

"Watoto tunashangaa haya yanayofanyika wakati hayana ridhaa ya jamii, sheria wala maadili kwanini yaendelee?

Anahoji kama inafahamika kuwa watoto wanatumiwa ili baadhi ya watu wapate mafanikio maana yake ni nini?

"Ni kuwaangamiza watoto au sisi binadamu wenzenu mkitumia nguvu za ushetani, ushirikina na uchawi ili muwe matajiri, vyeo vikubwa kisiasa na kwenye sehemu za kazi, au muwe na nguvu za kiume? Anahoji mwanafunzi huyu wa darasa la saba.

Anasema kinachotafutwa hapo ni laana na wala si mafanikio. Kama taifa linapaswa kuchunguza wanaochangia kuendeleza uovu huo, kuwakamata na kuwashtaki, kukemea uovu huo wa kujitafutia mafanikio kwa njia uovu na zisizokubalika kijamii.

**FIKRA MGANDO**

Msomi wa Saikolojia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii ya Dar es Salaam, (jina tunalo), anaeleza kuwa kinachoendelea katika kuamini ushirikina ni baadhi ya Watanzania kuwa na akili na fikra mgando.

Anaonya kuwa kuendelea kuwaza kuwa ili kupata utajiri, ubunge, nguvu za kiume, bahati na mafanikio ni sharti uwaumize watoto au binadamu wengine ni kuendelea kuwaza kizamani na kimgando licha ya kwamba hakuna ukweli.

Duniani kote watu wenye akili timamu wanafahamu kuwa kuua ni hatia na kumwaga damu ni kosa kubwa la jinai na adhabu yake ni kifo inakuwaje tena kiwe chanzo cha mafanikio?

Anasema ni jambo linaloshangaza kuona kuwa Watanzania wenye akili timamu na nguvu za kufanyakazi wanaridhika na kuamini kuwa njia za kishirikina za kuwaua na kuwanyanyasa watoto ndizo mbinu za kutafuta mafanikio kazini, kisiasa, kimapenzi, kiuchumi au kwenye ujasiriamali.

"Inashangaza kuutafuta utajiri au kufanikiwa kicheo, kisiasa, kupona magonjwa au kupanda cheo kazini shurti umwage damu ya mwenzako? anahoji mhadhiri huyo.

"Ni aibu kubaki na ujinga na mawazo duni kuwa ili kutajirika, kuibuka kisiasa, kuwa na afya njema ni lazima uwasilishe mtoto mdogo atolewe kafara, viungo vya albino, vipara au kumchuna mtu ngozi?"

Niwaulize hivyo viungo vinapatikanaje bila kuua? Kuteka watu, kutesa na kuwaumizia kiakili na kisaikolojia?

"Ni vizuri katika siku hii ya mtoto wa bara hili na Tanzania kutafakari jinsi mamia ya watoto na albino walivyofikishwa kwenye mauti, ulemavu au mateso ya kudumu kutokana na ushetani wa kuusaka utajiri," anaonya.

**KURUHUSU UGANGA**

Mwalimu huyu anaonya kuwa mambo hayo yanatokana na kuruhusu waganga, wapiga ramli na matabibu kuzagaa kila mahali na hata kupewa vibali wafanye kazi ambazo hazina tija.

"Wenzenu Amerika, Ulaya na China wanategemea sayansi na tekinolojia, hebu na sisi tutumie teknolojia kupata mafanikio badala ya kuendekeza fikra mgando za kuwategemea waganga na wapiga ramli ambao wengi ni mambumbumbu ," anashauri.

Anashauri jamii ikumbushwe kuachana na njia za mkato za kupata mafanikio na hasa masuala yanayohusu mauaji ya binadamu na watoto kwa sababu hatawakipata wanachotaka hawatafika mbali.

Anaonya kuwa kuendelea kufanya hivyo kunailazimisha jamii kufanya mambo kinyume cha ubinadamu, mila, imani za dini, maadili na miiko ya binadamu.

Lakini anaonya kuwa cha kutisha zaidi ni baadhi ya 'madalali' wanaotumiwa kwenye dili za kuwatesa na kuwaangamiza watoto ni wazazi, ndugu au jamaa wa karibu, walezi na hata watoto wenzao.

Anasema ni hatari kama baba, mama au mjomba, anawapiga bei au kumnadi, mwanae, mdogo wake, jirani au mwanafamilia yeyote kwa wenye tamaa za kupata utajiri au mfanikio ya haraka ya kutumia nguvu za giza.

NA BEATRICE PHILEMON

### SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Mwalimu anavyowapa neno la kusimamia watoto wake

KILA mwaka Juni 16, Bara la Afrika huadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika iliyoidhinishwa na Umoja wa Afrika (AU) mwaka 1991.

Umoja wa Afrika ulianzisha Siku ya Mtoto wa Afrika kama sehemu ya kuwakumbuka na kuutambua mchango wa watoto waliopoteza maisha katika mauaji yaliyotokea huko Soweto, Afrika ya Kusini.

Mauaji yalitokea wakati watoto walipoandamana kudai haki zao za msingi hasa elimu ili wafundishwe katika mazingira jumuishi badala ya kufundishwa kwa kutumia lugha za asili.

Mwaka huu maadhimisho hayo yanafikia miaka 29. Nipashe inazungumza na Stephen Mlobi (pichani), Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kilindoni iliyoko wilaya ya Mafia mkoani Pwani.

Anazungumzia masuala mbalimbali ikiwamo jinsi ya kuwalinda na kuwasaidia watoto kwani wanakabiliwa na changamoto nyingi bila kujali wanaishi mijini au vijijini.

Anasema katika kuhakikisha kwamba maadhimisho haya ya Siku ya Mtoto wa Afrika yanafanyika, kila mwaka yapo mashirika mbalimbali ya kiserikali na ya kijamii ambayo yanaungana na jamii ya Afrika kuadhimisha siku hiyo maalumu.

Lengo ni kushirikiana katika kutambua mchango wa watoto ndani ya jamii sambamba na kuamsha uelewa wa wadau kushiriki kikamilifu katika kutetea haki za watoto ikiwamo haki ya elimu na haki nyinginezo.

**CHANGAMOTO ZA WATOTO**

Mlobi anasema ni wazi kuwa siku hii maalumu inayoadhimishwa barani kote inafanyika wakati bado zipo changamoto kadha wa kadha ambazo watoto wengi wanakabiliana nazo.

Hizi ni pamoja na suala zima la mila potofu na ukandamiza pamoja kuwanyanyasa mabinti kwa kuendeleza mila na desturi za kuwakeketa.

Ukeketaji ambao sehemu nyingine umekuwa ukifanyika hata wakati huu wa likizo ya corona unaathiri mabinti katika mikoa mingi ikiwamo wa Mara hasa wilayani Serengeti. Katika maeneo hayo wadau wameshirikiana na polisi kuzima matukio ya unyanyasaji huo wa kimila.

Kwa mikoa yenye kushikilia mila hizo potofu maadhimisho haya ni vyema yakawa sehemu au fursa ya kufanya uhamasishaji kupinga ukatili kwa watoto hususani mila hiyo ya ukeketaji ambayo imeathiri kwa namna nyingi maslahi ya wasichana.



Sada Hatibu, mwanafunzi wa darasa sita katika Shule ya Msingi Kilindoni, akielezea jinsi ya kujua haki za watoto kunavyosaidia kutatua changamoto zinazowakabili nyumbani na shuleni. PICHA: BEATRICE PHILLEMON.

> "Niseme tasnia ya habari imekuwa mstari wa mbele katika kuripoti matukio ya namna hiyo na hatimaye vyombo vya dola kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya hao waharibifu wa watoto ambao ni taifa la leo na kesho."

**VIPI NDOA UTOTONI?**

Aidha, Mlobi anaikumbusha jamii kuwa inapaswa kutambua, kuheshimu na kulinda haki za watoto kwa kuzingatia kwamba haki za watoto zimekuwa hatarini kama vile vitendo vya ubakaji,mimba ,ndoa za utotoni na ukatili wa kimwili.

Vitendo vyote hivyo vingine vimekuwa vikifanywa na jamaa pamoja na ndugu wa karibu kwa watoto, hivyo kupelekea ugumu katika kufuatwa kwa sheria na kuzifikisha kesi hizo mahakamani.

Kunakuwa na ugumu kwani majadiliano na usuluhisho mara nyingi huishia katika ngazi za kaya na familia na mambo huisha bila watuhumiwa kuadhibiwa huku watoto wakiendelea kuumizwa.

Wakati mwingine kutokana na mambo kufanyika kwa misingi ya muhali au kuoneana aibu, kuogopa kuharibiana au kulindana wanajamii hushindwa kutoa ushahidi kwa kuoneana aibu dhidi ya watuhumiwa.

Wakati huu serikali iko makini , hivyo walimu , walezi na wadau wa ustawi wa watoto wanapenda kuishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuuwa mstari wa mbele zaidi katika kulinda na kusimamia haki za watoto.

Imekuwa mstari wa mbele hasa panapobainika kwamba kuna tatizo, hatua za haraka zimekuwa zikichukuliwa ili kumkomboa mtoto huyu ambaye ndoto zake zilielekea kuzimwa au kukatishwa.



Katika kuiunga mkono serikali jamii inapaswa kuwa bega kwa bega na serikali kwa nguvu zote katika kuwafichua watu ambao wanashiriki kukatisha ndoto za watoto hawa.

Sisi wenyewe tunajionea hapa nchini ambako ipo baadhi ya mikoa ambayo vitendo hivi vya ukatili vimekithiri na huwa vinatokea mara kwa mara.

**KWA WANAHABARI**

Mwalimu huyu anazungumzia kazi kubwa ya kutetea watoto inayofanyika kwa ushiriano na vyombo vya habari.

" Niseme tasnia ya habari imekuwa mstari wa mbele katika kuripoti matukio ya namna hiyo na hatimaye vyombo vya dola kuchua hatua kali za kisheria dhidi ya hao waharibifu wa watoto ambao ni taifa la leo na kesho."

**USHAURI S/MITAA**

Nisema katika kuhakikisha kuwa hayo yote yanafanikiwa natoa rai kwa serikali za mitaa kwa kutambua kuwa zinao wajibu wa kulinda na kutetea maslahi ya mtoto katika eneo husika iwe mtaani, kitongoji, kijijini au popote kupitia kwa maofisa ustawi wa jamii. Tunazishauri serikali za mitaa zishirikiane na Jeshi la Polisi katika kuwatafuta wazazi, walezi na ndugu wa watoto wanaohitaji msaada.

Lengo ni kuwapatia watoto malezi yaliyojengwa katika misingi bora na kuhakikisha kuwa wanakuwa salama na si kuangukia katika mikoa ya wanaowanyanyasa.

**UNAWAAMBIAJE WAZAZI?**

Ni muhimu pia kwa walezi, wazazi na jamii kuwalinda watoto. Aidha wanalo jukumu la kuwalinda watoto kwa kuwazuia kushiriki au kwenda kwenye maeneo ambayo yanaweza kusababisha vitendo viovu kufanyika dhidi yao.

Kwa mfano, katika maeneo ya vibanda vya kuonyesha picha au sinema . Hili si eneo salama watoto hujifunza upotevu na mambo maovu zikiwamo picha za ngono na hata kushawishiwa kufanya matendo ya kujamiiana.

Halikadhalika ni vyema wazazi kufuatilia zawadi zinazotolewa kwa watoto hasa kutoka kwa watu wasiofahamika kwa wazazi au walezi wa watoto hao.

Hatua ya kufuatilia na kudhibiti itasaidia kuweka utaratibu mzuri na salama wa watoto kwenda na kurudi shule kwa maeneo au vijiji ambayo shule zipo mbali na makazi ya wananchi au vijijini ili kuwalinda watoto na watu wabaya wanaotumia umbali huo kuwatendea uovu watoto.

**WADAU WENGINE**

Ni vyema pia kushirikiana na wadau kama madereva wa boda boda ambao ndiyo wasafirishaji wakubwa wa watoto. Hawa washirikiane na jamii kuwa walinzi wa amani, usalama wa wasichana na watumike kama mtandao wa kutoa taarifa polisi na kwa viongozi kuhusu matendo ya unyanyasaji watoto.

Aidha, wanaweza kuwa na taarifa muhimu kuhusu maadui au watesi wa watoto kwa kuwa ndiyo wanaotumiwa kuwabeba watoto katika safari mbalimbali.





# Ukarabati skimu ulivyoongezeka kwa miaka mitano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imejenga na kukarabati jumla ya skimu 179, za umwagiliaji na kufanikiwa kuongeza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 461,000 mwaka 2015, na kufikia 694,715 mwaka 2020.

Hayo yalielezwa juzi na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Daudi Kaali, wakati alipokuwa akitoa taarifa yake kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba.

Kaali alisema kati ya skimu zilizojengwa na kukarabatiwa 56, zinasubiri kuzinduliwa na mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa tija ya uzalishaji katika skimu zilizoendelezwa, ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 hadi 2.0 kwa hekta hadi kufikia wastani wa tani 4.0 hadi 5.0 kwa hekta ya zao la mpunga.

"Zao la mahindi uzalishaji umeongezeka kutoka tani 1.5 hadi tani 3.7-5.0 kwa hekta, vitunguu kutoka tani 13, hadi 26 kwa hekta na nyanya kutoka tani 5 hadi 18 kwa hekta na hivyo sekta ya umwagiliaji kuchangia asilimia 24, ya mahitaji yote ya chakula nchini," alisema Kaali.

Alisema mafanikio hayo yametokana na kutekelezwa kwa mradi wa kuendeleza wakulima wadogo ambao ulitekelezwa katika awamu tatu katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini.

"Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu ulighalimu Sh. bilioni 15.37 na ulihusisha ujenzi na ukarabati wa skimu 48, za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 13,722," alisema.

Pia alisema awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo ulihusisha ujenzi na ukarabati wa skimu 61, za umwagilijai zenye ukubwa wa hekta 22,312 uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 20.

Vile vile, alisema katika awamu ya tatu ya mradi huo utekelezaji wake ulihusisha ujenzi na ukarabati wa skimu 16, za umwagiliaji SSIDP ambapo skimu tisa, kati ya 16 za awamu ya tatu zimekamilika.

"Mradi huu hadi kukamilika unategemewa kugharimu jumla ya Sh. bilioni 6.36 ambapo jumla ya hekta 1,090 zinategemewa kuongezeka," alisema Kaali.

# Shirika lahofia watu wenye ualbino Oktoba

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalojihusisha na utetezi wa haki kwa watoto, vijana na watu wenye ulemavu wa ngozi (Foundation for Disabilities Hope), limeiomba serikali kutoa adhabu kali kwa watakaobainika kujihusisha na mauaji pamoja na ukataji wa viungo vya watu watu hao kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Ombi hilo lilitolewa na mwasisi wa shirika hilo, Michael Hosea, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya kimataifa ya kuongeza uelewa kuhusu ualbino mwishoni mwa wiki.

Hosea, alisema ni ukweli usiopingika baadhi yao wenye ualbino katika kipindi hiki cha uchaguzi wa urais, ubunge na udiwani maisha yao yapo hatarini kutokana na kuhofia kuuawa na kukatwa viungo vyao kwa imani za kishirikina zinazofanywa na waganga wa kienyeji.

"Hapa lazima nisime ukweli mtupu mbele ya Watanzania kwamba watu wenye ualbino wanakutana na changamoto nyingi za ukatili dhidi yao, hasa katika kipindi ambacho tunachoelekea cha uchaguzi ambacho kwa upande wao huwindwa kama wanyama wakati wao ni wanadamu," alisema.

Alisema mara zote imani na mila potofu zinazoongozwa na imani za ushirikina ndiyo zinazosababisha kuwapo na manyanyaso, kutengwa na jamii, unyanyapaa, ubaguzi na hata kufikia hatua ya mauaji miongoni mwao.

Kutokana na unyama huo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Damass Mukassa, akizungumza kwenye kilele cha siku ya maadhimisho hayo aliziomba taasisi mbalimbali na watu binafsi kutoa ajira kwa watu wenye ualbino ili wajikwamue kiuchumi.

Alisema kuwa kwa uwezo walionao wa kufanya kazi wanaweza kupatiwa nafasi ya kuajiriwa na hatimaye wakajikwamua na kuondokana na utegemezi ambao umejengeka kuwa wao kazi yao ni kuomba msaada kila wakati.



Mkazi wa Kizota, Mzee Jonathan Mazengo (80), akiperuzi vichwa vya habari kwenye magazeti yaliyokuwa yakiuzwa katika Mtaa wa Soko Kuu la Majengo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA** .

# Elimu ya kinga corona kuendelea

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

MRATIBU wa kampeni ya usafi wa mazingira na Ofisa Afya wa Wilaya ya Chamwino, Asha Mwasenga, amesema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga na maambukizo ya corona kwa kuwa baadhi ya watu maeneo ya vijijini hawaamini kuwa ugonjwa huo upo.

Mwasenga aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na mradi wa kutoa elimu kuhusiana na corona unaoendeshwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Woman Wake Up (WOWAP) kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society.

Alisema elimu kwa jamii itaendelea kutolea kwani bado kuna watu hawaamini kuwa ugonjwa huo upo.

"Ugonjwa huo upo na tutaendelea kuishi nao, tunawaelimisha wananchi hata wanapokuja kwenye vituo vya afya na maeneo mbalimbali, tunaendelea kushikamana kutoa elimu ili kupambana na hili janga," alisema.

Alisema pamoja na juhudi za kutoa elimu bado kuna changamoto za namna ya uvaaji sahihi wa barakoa.

"Mtu anakwenda zahanati bila barakoa ukimuuliza anasema kama sina hela ya kununua barakoa nifanyeje? Jamani lazima tujilinde ugonjwa huu upo na utaendelea kuwapo," alisema.

Alisema wananchi waendelee kuelimishwa jinsi ya kuvaa barakoa kwa usahihi.

"Unachukua barakoa unaingiza kamba yake kwenye sikio la kwanza kisha la pili, hakikisha pua na mdomo vimezibwa, yale marinda ya barakoa yanatakiwa kutazama chini ni kinga ya uchafu kama kirusi akija anakaa kenye mashimo ya marinda," alisema.

Alisema barakoa za kitambaa ziweke katika hali ya usafi zifuliwe, zianikwe juani kisha zipigwe pasi.

Mtendaji wa Kata ya Manchali, Bertha Muhibu, alisema unapotokea msiba watendaji wamekuwa wakipata shida sana, wananchi wanakusanyika kwa makundi wakiambiwa watawanyike hawaelewi.

"Sasa kuna utaratibu umewekwa kudhibiti mikusanyiko ya aina hiyo," alisema.

Alisema kama kata walishatoa maelekezo kuwa hairuhusiwi kukaa na maiti kwa zaidi ya siku mbili.

"Tunazuia mikusanyiko kwa kushirikiana na mgambo, kila kijiji kina mgambo watano miongoni mwa kazi zao ni kuondoa watu kenye mikusanyiko, inapotokea kifo cha mhisiwa wa corona utaratibu wa kuchukua sampuli hufanyika kwa haraka kwa mamlaka husika," alisema.

Shekhe Shaban Mbaruku wa msikiti wa Chalinze alisema anajitahidi kutoa elimu kwa waumini hasa kwenye suala la kuhakikisha anavaa barakoa, kukaa kwa umbali na hata kutopeana mikono.

"Kuna msiba moja nilihudhuria, watu bado wanapeana mikono, watu lazima wafuate maelekezo ya kujikinga yanayotolewa, alichosema Rais John Magufuli ni kuwa ugonjwa umepungua lazima tuendelee kuchukua tahadhari," alisema.

Alisema wanaokenda kwenye ibada kwenye misikiti wamekuwa akifuata taratibu zinazotakiwa, tunakaa umbali wa mita mbili kutoka mtu mmoja hadi mwingine na kuondoa dhana ya kupeana mikono wakati wa kutoka kwenye ibada.

"Hata kabla ya corona, misikitini tulikuwa tukinawa mikono lakini bila sabuni, sasa tunanawa kwa sabuni, tutaendelea kutoa limu na msisitizo juu ya maradhi ya corona na kuomba dua." alisema

Mtendaji wa Kijiji cha Manchali 'A', Wilaya ya Chamwino, Mathew Sudi, alisema kuna utaratibu umewekwa kenye vilabu vya pombe za kienyeji.

"kila kilabu cha pombe za kienyeji kinatakiwa kuwa na ndo, maji na sabuni kwa ajili ya kunawia mikono, pia kila mnywaji anatakiwa kuwa na lita yake ya kunywea na si kupokezana," alisema.

# Tulia awapiga jeki wananchi Kifunda ujenzi kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Kifunda, Kata ya Lufilyo, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wamemshukuru Naibu Spika wa Bunge, Tulia Ackson, kwa msaada wa vifaa vya ujenzi ikiwamo mabati 100 na mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo juzi, Meneja Taasisi hiyo, Jacqueline Boaz, alisema walihamasika kuchangia kutokana na jitihada walizozifanya wananchi hao wa Kifunda kuamua kujenga kituo cha afya.

Boaz alisema hadi sasa taasisi hiyo ilitoa mifuko 100 ya saruji na mabati 100 ili yasaidie kukamilisha ujenzi, huku akiwahamasisha wananchi kuendelea kujitoa kukamilisha ujenzi.

"Tumekuwa tukikitembelea kituo hicho mara kwa mara kuangalia maendeleo ya kituo hiki na sisi tulihamasika na kuchangia, nawapongeza wananchi wa Kifunda kwa kujitolea nguvu kazi zao mmefanya kitu kinaonekana nawaomba mwendelee kujitolea ili kukamilisha na kusaidia kuondokana na adha mnayoipata," alisema Boaz.

Akitoa shukrani kwa msaada huo, Mtendaji wa Kijiji hicho, Huruma Kamala, alisema ujenzi huo ulianza mwaka 2017 ukitekelezwa na wananchi 368 kwa kushirikiana na Taasisi ya Tulia Ackson na kwamba hadi sasa wamekamilisha jengo la wagonjwa wa nje (OPD) lenye vyumba 17 na kati ya hivyo 10 vilisakafiwa na vingine saba wanaendelea navyo.

Alisema tatizo linalokwamisha kwa sasa ni ukata wa fedha licha ya kuwa bado wanaendelea na ujenzi kwa kujitolea fedha na mali ili kukamilisha na kuwaomba wadau wengine kujitoa kusaidia.

Aliongeza kuwa hadi sasa jumla ya Sh. milioni 100 zilizochangwa na wananchi zimetumika kujenga kituo hicho.




Ofisa Habari wa Shamba la Kapunga Rise Project, James Malick (kulia), akipokea cheti cha shukrani kwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Brown Mwakibete, baada ya shamba hilo, kuchangia fedha Sh. milioni 750, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kapunga katika kata ya Itamboleo, wilayani Mbarali mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Mbarali yasajili zaidi ya watoto 40,000 Rita

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WATOTO wenye umri chini ya miaka mitano 41,620 walioko Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wamesajiliwa na kuingizwa kwenye mfumo kupitia Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (Rita) katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Mipango wa Wilaya ya Mbarali, Emmanuel Kishimbo, idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na lengo walilojiwekea la kusajili watoto 57,916 hadi kufikia mwezi Mei 2020.

Alitaja miongoni mwa vikwazo vilivyochangia kusuasua kuwa ni mitandao ya mawasiliano wakati mwingine kutofanya kazi hivyo kusababisha wateja kutopata vyeti kwa wakati.

Alisema baadhi ya wasajili waliopo kwenye ngazi ya kata kukosa mawasiliano na husababisha ucheleweshaji wa zoezi, pia uhaba wa fedha za kufanya uhamasishaji wa kutosha katika jamii.

"Halmashauri imejitahidi kuhamasisha wananchi hususani wazazi kuwaandikisha watoto mbali na kuwaandikisha walio na umri chini ya miaka mitano, lakini wenye miaka zaidi ya mitano 3,371 na jumla ya vyeti 98 vya vifo vilitolewa na mwenendo wa usajili kuanzia ngazi ya kata 20 na vituo 46," alisema Kishimbo.

Alisema katika jitihada za kukabiliana na vikwazo hivyo, wanaendelea kufanya mawasiliano na wataalamu wa mifumo wa kompyuta pamoja na kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha Rita na wilaya kufanikisha uhamasishaji.

Katika hatua nyingine, Kishimbo alisema Idara ya Maendeleo ya Jamii kupitia mpango wa kudhibiti Maambukizo ya Virusi vya Ukimwi kwa mwaka 2019/20 umesaidia kuimarisha na kuanzisha klabu za kudhibiti maambukizo kwenye shule za sekondari 23 na msingi 52 ambazo tayari zina walimu waliojengewa uwezo.

Alisema wilaya kwa kushirikiana na asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali, iliwezesha upatikanaji wa elimu katika jamii, upimaji wa VVU na uanzishwaji wa vikundi vya kiuchumi na kusajiliwa ambapo jumla ya vikundi 60 vyenye kaya maskini zenye kuishi na watoto yatima zimeendelea kunufaika.

# Tari yawashauri wakulima kutumia mbegu bora

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), imewashauri wakulima kuacha tabia ya kutumia mbegu za zamani ambazo hutoa mavuno haba, huku wakibeza mbegu mpya zilizofanyiwa utafiti kwa madai ya kuharibu afya ya udongo.

Iliwahimiza wakulima kote nchini kufika kwenye vituo vya utafiti vilivyo karibu ili kupata mbegu bora zinazoendana na mazingira yao badala ya kuendelea na matumizi ya mbegu za zamani.

Hayo yalithibitishwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Godfrey Nkamilo, alipotembelea Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole.

Ni wakati sasa wakulima kutumia teknolojia mpya za kilimo ikiwamo mbegu ili kuongeza mavuno yatakayosaidia kujiongezea kipato na kumudu gharama za maisha.

"Afya ya udongo ni mpango mzima ni muhimu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao nawashauri wakulima nchini kufuata maelekezo ya watafiti na wataalamu, kuna kituo cha utafiti kiko pale Tanga kinaitwa Mlingano kinajihusisha na afya ya udongo matumizi bora ya ardhi na mbolea," alisema Dk. Nkamilo.

Aliongeza kuwa Tari Uyole imekuwa ikitoa teknolojia mbalimbali za kiutafiti ili kuwasaidia wakulima kwa kutumia mashamba darasa kwa wakulima na maonyesho ya kibiashara ya kilimo, mathalani katika eneo la teknolojia ya utumiaji wa mbegu bora za mahindi ambayo hupandwa katika eneo dogo na kuwa mavuno mengi.

Mkurugenzi wa Tari Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kuwapo kwa kituo hicho cha utafiti masuala ya kilimo mkoani Mbeya kunalenga kuleta tija kwa wakulima wanaotumia teknolojia mbalimbali za kitafiti.

Alisema miaka ya nyuma walijikita kufanya utafiti wa teknolojia mbalimbali za mbegu na kwamba sasa ni wakati wa kuzitumia kwa kuwa zimeleta tija kwenye maeneo kama vile shamba darasa.

**Afya ya udongo ni mpango mzima ni muhimu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao nawashauri wakulima nchini kufuata maelekezo ya watafiti na wataalamu, kuna kituo cha utafiti kiko pale Tanga kinaitwa Mlingano kinajihusisha na afya ya udongo matumizi bora ya ardhi na mbolea**

# Balozi Iddi ataja wanaofaa kuwania uongozi Oktoba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Seif Ali Iddi, amesema wakati muda wa kuelekea katika uchaguzi mkuu unakaribia wana-CCM na wananchi wana fursa nzuri ya kutafakari kiongozi atakayefaa kuwaongoza katika kipindi kijacho cha miaka mitano.

Alisema viongozi wanaofaa kushika hatamu ya kuwaongoza vyema ni wale wenye uwezo kamili wa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM inayokwenda kisasa katika mazingira ya karne ya sasa ya sayansi na teknolojia ulimwenguni.

Balozi Iddi ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alitoa kauli hiyo akimwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein katika uzinduzi wa tangi kubwa la kuhifadhia majisafi na salama pamoja na uzinduzi wa ifisi ya Jimbo la Kikwajuni iliyofanyiwa matengenezo makubwa ikiwa ni umaliziaji wa utekelzaji wa ilani ya uchaguzi katika jimbo hilo.

Alisema wananchi wanapaswa kufanya tathmini ya kina itakayoweza kuwaibulia mchapakazi imara atakayejitolea kusimamia kwa wakati wote masuala yao ya maendeleo na uchumi katika maeneo yao.

Alieleza kwamba kumchagua kiongozi kabla ya kumfanyia uhakiki wa kina huleta hatari kwani matokeo yake ni majuto yasiyokuwa na suluhu na hata kama uchaguzi ukiambatana na rushwa inayokuwa kaa la moto ndani ya miaka mitano.

"Wagombea waliopenya na wale watakaopenya kwenye kampeni kabla ya wakati chama hakitosita kuwachukulia hatua za nidhamu ikiwamo kuwakata katika mchakato wa kumtafuta mgombea," alisema.

Balozi Iddi aliwataka wanachama wa CCM lazima waendelee kuwa na kauli moja itakayotoa nguvu ya ushindi ili CCM iendelee kushika dola.

Alielezea furaha yake kuwa kutokana na utekelezaji mkubwa wa Ilani ya Uchaguzi kwa Mwaka 2015 - 2020 uliofanywa na CCM hasa upande wa Zanzibar kwa vile haukupata vikwazo wala msukosuko kama ilivyokuwa 2010-2015 kutokana na wasimamizi wake kuwa na kauli moja katika utekelezaji huo.

Alisema CCM kupitia serikali zake zote mbili Tanzania Bara na Zanzibar bado kina dhima ya kuendelea kulinda amani na utulivu uliosaidia kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa maendeleo na kupigiwa mfano barani Afrika.

Aliwakumbusha wanachama wenye nia ya kuchukua fomu kwa ajili ya kuomba uongozi ndani ya CCM wazingatie sheria, muongozo na taratibu zilizowekwa.

Wakiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015-2020 Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni, Nassor Salum Jazira na Mbunge wa Jimbo hilo, Mhandisi Hamad Yusuf Masauni wamesema CCM kwenye uchaguzi ujao haitapata shida kuwanadi wagombea wake watakaopata fursa ya kuteuliwa kugombea jimbo hilo.

Walisema hiyo inatokana na utekelezaji mkubwa wa ilani ya uchaguzi Jimbo la Kikwajuni Wilaya ya Mjini ambayo imepindukia kwa asilimia 100.

Katibu wa CCM Jimbo la Kikwajuni, Farid Abdullah Hamad, alisema kwa niaba ya wanachama na wananchi wa jimbo hilo wanaishukuru Serikali Kuu hatua kubwa ilizochukua ya kuimarisha miundombinu mingi ya maendeleo katika jimbo hilo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, akizungumza na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi wa Jimbo la Kikwajuni, baada ya kuzindua rasmi tangi kubwa la kuhifadhia majisafi na salama pamoja na ofisi ya jimbo hilo, jana. **PICHA: OMPR – ZNZ.**

# Asasi zashtushwa udhalilishaji watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ASASI za kirai visiwani Zanzibar zimesema kuna idadi kubwa ya matukio ya udhalilishaji kwa watoto, hali ambayo inaweza taifa kukosa wataalamu katika miaka ijayo.

Akiwasilisha ripoti ya asasi hizo Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Dk. Sikujua Omar, alisema kuna matukio 1,0490 katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba yameripotiwa tokea mwaka 2017 hadi mwaka 2019.

Akitolea ufafanuzi wa kesi hizo, alisema kesi hizo ambazo zimetolewa hukumu kutoka mwaka 2017 hadi sasa ni 404 wakati kesi 704 zinaendelea na upelelezi na kesi 266 watuhumiwa hawakukutwa na hatia wakati kesi 59 zilikutwa na hatia.

Akitaja sababu za uwapo wa matukio hayo alisema ni baadhi ya wanajamii kutokuwa makini na malezi ya watoto wao sambamba na kuwanunua vitu visivyokuwa muhimu na vinavyoweza kujenga ushawishi kwa watoto.

Pia alisema baadhi ya wanajamii kutokuwa na uelewa kuhusu matendo ya udhalilishaji na kuhisi kuwa ni vitu vya kawaida na ndio maana hushindwa kuwadhibiti na kuwafuatilia watoto wao majumbani.

Alieleza kuwa imekuwa kawaida kwa baadhi ya wazazi au walezi kuwafungulia milango watoto wao wa kike saa tano za usiku kwa kisingizio cha kujisomea elimu ya ziada (tuisheni).

Alisema mazingira hayo nayo pia ni sehemu hatarishi kwa watoto kufanyiwa udhalilishaji, na kwamba wazazi au walezi wanapaswa kukataa mwenendo wa watoto wao.

Naye Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mohamed, alisema ipo haja kubwa wakati Afrika ikielekea kuadhimisha siku hiyo jamii kubadili tabia na kutambua umuhimu wa mtoto.

Alisema kuwekwa kwa siku hiyo mahsusi ililenga kutambua umuhimu wa mtoto wa Afrika na kwamba wanapaswa kutunzwa na kuenziwa na kupewa haki zote.

Kwa upande wake Meneja miradi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) upande wa Zanzibar, Asha Abdi, alisema kuna mazingira magumu ambayo watetezi wa haki za watoto wamekuwa wakikutana nayo hususani kwenye kufuatilia kesi zao.

## Wanaharakati waipa tano ofisi ya Mufti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAHARAKATI wa kutetea haki za watoto wameipongeza Ofisi ya Mufti ya Zanzibar kuifungia madrasati Ridhwaa Madihi Rassuli iliopo Jang'ombe Unguja kwa madai ya kuwapo tuhuma za vitendo vya udhalilishaji kwa wanafunzi.

Wakizungumza na Nipashe, walisema walimu wa madrasa hiyo wanatuhumiwa kuwalawiti baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho.

Meneja wa Utetezi wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) upande wa Zanzibar, Salma Lusangi, alisema wanaunga mkono uamuzi huo ambao lengo lake ni kukomesha matukio hayo yanayodhalilisha watoto ambao wapo chini ya dhamana za walimu.

Lusangi alisema Tamwa kwa muda mrefu ilikuwa ikifuatilia suala la kuwapo kwa tuhuma za vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vinavyofanywa katika madrasati kwa upande wa Unguja na Pemba.

Alisema Tamwa imefanya uchunguzi na kubaini kuwapo zaidi ya wanafunzi 20 waliofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kinyume cha maumbile.

"Tamwa tunaunga mkono uamuzi uliochukuliwa na Ofisi ya Mufti kuifungia madrasati hiyo kwa tuhuma za vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanywa na walimu na wanafunzi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jamila Mahmoud, alisema ni hatua nzuri uchunguzi zaidi ufanyike kwa madrasa nyingine ambazo zinalalamikiwa kuhusiana na matukio hayo.

Alisema matukio ya vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto yamekithiri na kusababisha hofu kubwa kwa jamii ya wazazi Unguja na Pemba.

"Zafela kimefurahishwa na juhudi zilizochukuliwa na ofisi ya Mufti kuifungia madrasa iliyopo Jang'ombe kwa tuhuma za kuwapo kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanafunzi na walimu,'' alisema.

Mwishoni mwa wiki iliyopita Katibu wa Mufti, Khalid Ali Mfaume, alitangaza kuifunga madrasa hiyo kwa tuhuma za kuwapo kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ukiwamo ubakaji na ulawiti.

Khalid alisema katika mwaka 2011 Ofisi ya Mufti ilipokea malalamiko sita ya udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto wa kiume kulawitiwa na walimu wao wa madrasa.

Katika tukio hilo ofisi ya Mufti imewafutia leseni ya kusomesha madrasa jumla ya walimu sita kwa tuhuma hizo, huku wazazi wakitakiwa kuwapeleka sehemu nyingine watoto wao kupata elimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI YA DEREVA NA MAUZO** Mwenye uzoefu wa kuuza Maji. PIga simu namba : **0767 269677 saa za kazi**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

***PUBLICATION SUMMONS***
**IN THE PRESIDENT MAGISTRATES' COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**

**TAXATION CAUSE NO: 03/2020**

**(Arising from Resident Magistrate court of Bukoba at Bukoba Civil Case No 9 of 2019**

**IGOMA KOLPING SAVING AND CREDT COOPERATION SOCIERT ………………………APPLICANT**

**VERSUS**

**JULIUS. M.APORINARY ……………………RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

**TO: JULIUS. M. APORINARY**

**TAKE NOTICE** that the mentioned case has been set down for Hearing on the 17th day of JUNE, 2020 at 8:30 o'clock in the forenoon, Before Hon. J.P.KAPOKOLO- SRM. your presence is therefore required on the date and the time indicated.

Given under my hand and the seal of the court this 01st day of JUNE. 2020

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
WITH EXTENDED JURISICTION
BUKOBA

115774502

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE RESIDENT MAGISTATE'S COURT OF BUKOBA AT BUKOBA.**

**TAXATION CAUSE NO. 03 OF 2020**
**(Arising From Civil Case No. 09 of 2019)**

**IGOMA KOLPING SAVING AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY ………………………APPLICANT**

**VERSUS**

**JULIUS. M APORINARY …………………RESPONDENT**

***Notice To Show cause why bill of costs should not issue***

**To: JULIUS. M. APORINARY**

Whereas the *plaintiff (Decree Holder) has made application to this Court for Bill of Cost in the Civil Case No 9 of 2019. This is to give you notice that you are to appear before this Court on the 17th day of June, 2020 to show cause why Bill of costs should not be granted

**GIVEN under my HAND** and the SEAL of the court, this 0**1st day of JUNE, 2020**

Registrar/Magistrate in charge

115774502

---

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**Katika Mahakama ya Mwanzo…… Mwanga**
**Wilaya ya Mwanga**

**Mirathi No, 09 …….2020**

**Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya Marehemu ZIADA SHABANI KISHANGA NA MUSTAFA NUHU KISHANGA MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji hapo juu Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe….15…/06/….2020 .

Imewasilishwa MWANGA leo tarehe 15 mwezi 04 mwaka 2020

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANGA

215776702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA NDOA NO.16 MWAKA 2020**

**MICHAEL NDUDUNGU…………….MDAI**

**DHIDI**

**JASMIN BAHASHA SALUGOLE……………..MDAIWA**

**KWA: JASMIN BAHASHA SALUGOLE**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya madai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii,kwa hiyo mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya tarehe 17/06/2020… saa 7:00 Mchana. Mbele yam h. H.A. SHAIDI-PRM.
**ANGALIZO:**
Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibtisha kama mmepotea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 12 mwezi wa sita,2020.

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM

115774802

---

## CHETI KIMEPOTEA



215775102

**STAFORD ADAM MBAGAYE** anatangaza kupotelewa na Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne Chenye **Index Number S.3963/0038** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya Sekondari Nyamtukuza iliyopo Kakonko, Kigoma. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilicho karibu. Au piga simu namba **0756-572224 au 0785-194972.** Taarifa ya Polisi: **MAG/CID/B.1/1/VOL.IX/04.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.34. 2020**

**In the matter of the Estate of the late BARAKA BISSE SENDI of Kigamboni Street, within Dodoma Region**

**AND**

**In the matter of an application for letters of Administration by ISAAC BISSE SENDI**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before the 01 Day of July 2020.
Dated at Dodoma this 16 Day of April 2020.

Presented for filling this 16 Day of May 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

215776601

---

**JAMUHURI & COMPANY ADVOCATES**
**Uhuru street plot No 7 Block 54, Kariakoo**
**Adjacent to CRDB, P O BOX 80386, Dar es Salaam**
**Mobile 0769 419332, 0654037913**
**Email: benedictpius71@gmail.com, bensonfloast@gmail.com**

**Ref: JCA/BM/01/16/20**
**MISS NURU RAMADHANI SWALEHE,**
**P.O BOX 2569,**
**DAR ES SALAAM**

**Date: 15th JUNE, 2020**

**RE: NOTICE TO VACATE FROM THE HOUSE No. 08-2C KNZ LOCATED AT PLOT NO. 268, KINYEREZI DAR ES SALAAM**

We are acting for and on behalf of **MR. ZAKARIA M. MHENGA** (Hereinafter our Client) with instruction to address you of the following;

1. That you have been occupying our client's house without valid agreement.
2. That you have failed to maintain and repair the said house to the extent that it has fallen into dilapidation hence become unfit for human habitation during your occupancy.
3. That our client has made various efforts to communicate with you, your workmen, agents and people acting on your behalf but all efforts has become futile.
4. That you're occurred to vacate the said house since our client intend to repair the said dilapidated house in order to reside therein.
5. That this Notice shall take effect within 14 days from the date of its issuances and you're required to vacate from the said house.

**TAKE NOTICE THAT,** In the premises we are writing this notice on behalf of our client, failure to comply with this notice within 14 days our clients will initiate legal redress without further notice.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT,** this notice shall include any other people claiming interest over the above captioned House.
Please be also guided by this notice

……………………………………………………
**B.F VEDAASTO**
**FOR: JAMUHURI & COMPANY ADVOCATES** Copy: client: as you instructed.

Advocate J.J. JOhhnson LL.B Hons. Notaries Public and commissioner for Oath, commercial and Business Lawyers, conveyancers

215776202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;144/2020**

**Ombi la ERNESTINA MAZURI MASALU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ROBERT MAGOLANGA KIYUMBI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 13/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/06/2020.

Tarehe 5/6/2020
HAKIMU

215776102

---

**DATED THIS……..DAY OF JUNE 2020**
**AFFIDAVIT REGARDING CITIZENSHIP**

**I ISMAIL MOHAMED CHAKULIMBA** Adult, Muslim and resident of Dodoma city do **HEARBY AFFIRM AND STATE** follows:

1. **THAT, I** was born in 1947 in Iringa District within Iringa Region
2. **THAT,** I am Tanzania by birth with Registered Citizen Identity card NO. 0947020541216-00001-29.
3. **THAT,** let be known that **I ISMAIL MOHAMED CHAKULIMBA,** I am a Citizen of Tanzania and not otherwise.

**VERIFICATION:** What is stated above is true to the best of my knowledge.

SOLEMNLY AFFIRMED by the said ISMAIL MOHAMED CHAKULIMBA who is known to me personally this……… day of June, 2020.



BEFORE ME

SIGNATURE: …………………

NAME: …………………
ADDRESS P. O. BOX 1013 DODOMA
QUALIFICATION: COMMISSIONER FOR OATHS

115776002

---

## LOST TITLE DEED

**I Anna Ngulumu Mdemu,** the owner of a little deed with **Registration number 1306-mbyr** which is on plot **No. 505, block D** located/situated Mafinga Urban area, is lost. Please if found return it to the nearest police station or please contact the following phone numbers**: 0657 310505, 0714 951168, 0714 431962. Police Report: UBS/RB/914/2020.**

115776302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;136/2020**

**Ombi la MALEZYA KAPYOLO MKANTULA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ISSA MAULID MAGANGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/06/2020.

Tarehe 2/6/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115775201

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**
**KIGOMA**

**MAOMBI NA. 52 MWAKA 2020**

**MRS ZUBEDA AHMED LAKHA………MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**HAJIBHAI KARA IBRAHIM……………MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: HAJIBHAI KARA IBRAHIM**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 09 Mwezi Juni Mwaka 2020 saa 2:30 Asubuhi mbele ya Mhe. F. CHINUKU, Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 22 Mwezi 5 Mwaka 2020.

F. CHINUKU
MWENYEKITI

115775302

---

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe

kila siku Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Kesi dawa kulevya yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

KESI ya uhujumu uchumi ikiwamo kusafirisha kilo 268.50 za dawa za kulevya na kutakatisha fedha inayokabili raia wa Nigeria, David Chukwu (38) na wenzake wawili imepigwa kalenda mpaka Juni 29, mwaka huu.

Upande wa Jamhuri ulidai kwamba kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini upelelezi bado haujakamilika.

Kesi hiyo imetajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Godfrey Isaya.

Wakili wa Serikali, Kija Luzungana, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuiomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa.

Hakimu Isaya alisema kesi hiyo itatajwa Mei 21, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Chukwu washtakiwa wengine ni Isso Lupembe (49), mkazi wa Mbezi na Allistair Mbele (38), mkazi wa Mbezi Kibanda cha Mkaa.

Ilidaiwa kuwa Aprili 15, mwaka huu eneo la Mbezi Kibanda cha Mkaa, washtakiwa wote kwa pamoja walikutwa wakisafirisha kilo 268.50 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa kati ya Januari mosi, 2016 na Aprili 15, mwaka huu washtakiwa walitakatisha fedha baada ya kujihusisha na miamala ya Dola za Marekani 61,500 na Sh. 17,835,000 huku wakijua ni zao la tangulizi la biashara ya dawa za kulevya.

## Polepole ataka vijana kugombea uongozi

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, amewaasa vijana kujitokeza na kushiriki kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wanafunzi wa vyuo vikuu na vya kati ambao ni wanachama CCM.

Pia, alifanya kikao cha ndani cha kimkakati na viongozi wa matawi ya vyuo wakiwamo wajumbe wa seneti jijini humo.

Polepole aliwataka vijana kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanakisemea vyema chama na serikali hasa kuelekea uchaguzi mkuu.

"Vijana ambao wana uwezo wajitokeze kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi huu mkuu nafasi za ubunge na udiwani maana vijana ni taifa la leo na kesho," alisema Polepole.

Katibu wa Seneti Mkoa wa Dar es Salaam, Daud Said, alisisitiza wanavyuo kuendelea kukijenga chama vyema kwenye matawi yao na kuwa imara zaidi kwenye kukisemea na kukipambania.

# Daftari wapigakura wazi kesho

**Na Fatma Mtutuma, UDOM**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza kuweka wazi daftari la awali la wapigakura kwa siku nne, kuanzia Juni 17 hadi 20, mwaka huu.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwenye magazeti, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, ratiba hiyo itafanyika kwa kuzingatia tahadhari zote za afya kwa ajili ya kuzuia maambukizo ya corona.

Alisema uwekaji wazi huo, utahusisha mambo mbalimbali ambayo ni wapigakura wote walioandikishwa katika daftari la kudumu la mpigakura mwaka 2015 na waliondikishwa wakati wa uboreshaji wa daftari la 2019/2020.

"Wapigakura hawa ni wale ambao hawakuhakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi daftari la awali la wapigakura awamu ya kwanza," alifafanua Dk. Mahera.

Vile vile, alitoa utaratibu wa uhakiki ambao mpigakura anaweza kuhakiki taarifa zake kwa utaratibu huo, katika uwekaji wazi wa daftari hilo.

"Mpigakura mwenyewe anatakiwa kufika katika kituo alichojiandikisha na kuhakiki taarifa zake katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika kituo hicho," alisema Dk. Mahera.

Mkurugenzi huyo alieleza zaidi kuwa, utaratibu mwingine ni mpigakura kuhakiki taarifa zake kupitia simu yake ya kiganjani.

Alisema daftari la awali la wapigakura pia litabandikwa katika vituo vyote vilivyotumika kuandikisha wapigakura, iwapo mpigakura amehakiki taarifa zake kwa kutumia njia yoyote na kutaka kufanya marekebisho.

"Mpigakura anayehitaji kumwekea pingamizi mpigakura asiye na sifa za kuwamo katika daftari la awali la wapiga kura ataenda katika kituo kilichopangwa katika halmashauri husika," alisema Dk. Mahera.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa, katika ratiba hiyo hakutakuwa na uandikishaji wa wapigakura wapya, uboreshaji wa taarifa za wapigakura waliohama maeneo yao ya kiuchaguzi na waliopoteza kadi au kadi zao kuharibika.



Fundi wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), akifanya marekebisho ya waya baada ya kutokea hitilafu kwenye nguzo katika eneo la Kitunda, jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wenye viwanda waifagilia bajeti

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda nchini (CTI), limepongeza bajeti ya serikali ya mwaka 2020/21 kwani imeyafanyia kazi malalamiko mengi yaliyotolewa na wafanyabiashara na wenye viwanda.

Pongezi hizo zilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti Msaidizi wa Shirikisho hilo, Paul Makanza, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu bajeti hiyo iliyosomwa Juni 11.

Alisema kwenye bajeti hiyo serikali imeondoa mlolongo wa tozo mbalimbali zilizokuwa zikilalamikiwa na wafanyabiashara na wenye viwanda hali itakayosaidia kuongeza tija.

Alisema serikali ya awamu ya tano imejitahidi kuweka mazingira mazuri ya biashara kupitia mpango wake wa Blur Print na imeweka mkakati wa kusisimua biashara na viwanda baada ya kutikiswa na ugonjwa wa corona.

"Serikali imetambua namna biashara na viwanda vilivyoathiriwa na ugonjwa wa corona sasa tunaipongeza kwa kuja na bajeti yenye mwelekeo wa kusisimua uchumi na biashara ziweze kurejea kwenye hali ya kawaida," alisema Makanza.

Aidha, alisema CTI iko bega kwa bega na serikali kuhakikisha mpango wake wa 2025 unafanikiwa na imeweka mazingira mazuri ili bidhaa nyingi ziongezewe thamani badala ya kuuzwa nje ya nchi zikiwa ghafi.

Makanza alipongeza hatua ya serikali kupunguza kodi ya kujengea uwezo na ujuzi (SDL) kutoka asilimia tano hadi nne na kwamba itasaidia kuongeza ajira na kulinda zile zilizopo. Alisema sekta ya viwanda imeendelea kukua miaka mitano iliyopita kwani viwanda 8,477 vikubwa, vidogo na vya kati vimejengwa, ambavyo vimesababisha ajira 482,601.

Kuhusu marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kwa wafanyabiashara wanaouza bidhaa zao nje ya nchi, alisema ingawa kuna deni kubwa, lakini serikali inajitahidi sana kulipa.

"Viwanda vingi vinavyouza nje havijalipwa ila tunaendelea kuzungumza na serikali kuona namna ya kumaliza deni hilo, lakini tunaona kuna nia ya kulipa kidogo kidogo," alisema.



# RONALDO

## AMEIPA JUVE MSUKUMO, ASEMA CHIELLINI

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo ameipa Juventus "msukumo mkubwa" tangu alivyotua klabuni hapo, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake, Giorgio Chiellini.

Ronaldo amefunga mabao 53 katika mechi 76 tangu alipojiunga na Juve akitokea Real Madrid mwaka 2018, akiwasaidia miamba hao wa Italia kushinda taji la Serie A msimu uliopita.

Nyota huyo wa Ureno ameiongoza klabu hiyo kileleni mwa msimamo wa Serie A msimu huu, huku wakiwa wametinga fainali ya Coppa Italia na wapo kwenye 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Chiellini amemsifia Ronaldo kwa kuisaidia Juventus kupiga hatua nyingine mbele, huku Bianconeri hao wakiangalia uwezekano wa kutwaa taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 1996.

"Ametupa msukumo mkubwa, kumfanya kila mmoja wetu kuwa kwenye ubora wake na kuipa msukumo jamii yote," amesema nahodha huyo wa Juve akimwambia Martina Colombari kwenye Instagram.

"Yeye ni wa daraja jingine kabisa, tunacheza kwa ajili yake na kumfanya awe na kiwango bora kabisa."

Juventus itacheza na Napoli kwenye fainali ya Coppa Italia mjini Rome kesho Jumatano.

# ZIDANE: HAZARD AMERUDI VIZURI

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane alikuwa na furaha kuona Eden Hazard akionyesha kiwango cha kuvutia wakati Real Madrid wakishinda mchezo wao wa LaLiga, akisema nyota huyo wa Ubelgiji alikuwa bora na amefanikiwa kumaliza changamoto zake.

Hazard alianza kwenye mchezo huo uliopigwa katika dimba la Alfredo Di Stefano Jumapili wakati Madrid wakishinda 3-1 dhidi ya Eibar na kuendelea kubakiwa ikipitwa pointi mbili na vinara wa ligi hiyo, Barcelona.

Majeruhi yalimkumba Hazard katika msimu wake wa kwanza na klabu hiyo tangu atue kwa ada ya euro milioni 100 kutoka Chelsea na ilionekana kama msimu huu kwake hatacheza tena baada ya kuumia kifundo cha mguu Februari.

Mlipuko wa virusi vya corona ukafanya ligi isimame kwa muda na yeye kupata nafasi ya kujifua na alionekana kuwa kwenye kiwango katika kipindi cha kwanza dhidi ya Eibar, akitengeneza bao la pili lililofungwa na Sergio Ramos na pia alitoa mchango mkubwa kwenye bao la tatu lililofungwa na Marcelo.

Hazard alikuwa akikabiliwa na changamoto kubwa na hivyo alitolewa nje dakika ya 61, lakini kocha wake, Zidane alionekana kuridhishwa na kiwango chake.

"Tulijua kwamba Eden angekosa ufiti wa kucheza mchezo wote. Lakini aliweza kucheza saa moja na alicheza vizuri," alisema.

"Walimpa ushirikiano mzuri. Alikuwa vizuri hadi mapumziko na alijisikia furaha kuonyesha kiwango chake na wala hakuwa na woga. Ana furaha na kile alichokifanya dimbani na sisi tunafuraha pia."




***

# IBRAHIMOVIC AKATALIWA BOLOGNA

**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimovic hana "uwezekano" kutua Bologna, mkurugenzi wa klabu hiyo, amethibitisha.

Mkongwe huyo alisaini mkataba wa muda mfupi kurudi AC Milan Jauari, lakini inaonekana ni wazi kwamba, Ibrahimovic hataweza kuendelea kukaa hapo kwenye dimba la San Siro msimu ujao.

Ibrahimovic amekuwa akihusishwa na Bologna kabla ya kujiunga na Milan, hasa kutokana na mahusiano yake mazuri na kocha mkuu wa klabu hiyo, Sinisa Mihajlovic – ambaye alikuwa kwenye benchi la ufundi pale Inter Milan wakati fowadi huyo akiwa na Nerazzurri hao, na ripoti ya kujaribu kumsajili raia huyo wa Sweden ilitoa wiki za hivi karibuni.



Lakini akizungumza mwezi uliopita, mkurugenzi wa klabu hiyo, Walter Sabatini alipinga wazo hilo na mkurugenzi wa michezo, Riccardo Bigon pia amebainisha kuwa hakuna nafasi ya kumsajili Ibrahimovic pale Bologna.

"Naelewa nia ya vyombo vya habari kwa kutengeneza habari hii, hasa kutokana na kuwa jina lake ni muhimu na lipo daraja la juu, lakini kwa upande wetu Ibrahimovic hana uwezekano wa kusajiliwa," alisema Bigon akiiambia redio RAI 1 kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38.

"Hatuna mawasiliano naye. Alizungumza na Mihajlovic kipindi cha majira ya baridi, na alifanya chaguo lake na kuanzia hapo hatujawahi kumfikiria tena."




# SANCHO

## ATAFITI ZAIDI MAN UNITED - SAHA

**MANCHESTER, England**

JADON Sancho anaweza kufiti zaidi pale Manchester United kwa sababu ya ubunifu wake na akili ya mchezo kutamfanya kuwa sehemu ya wachezaji muhimu wa klabu, amesema Louis Saha.

Uamuzi wa Sancho kuondoka katika akademi ya vijana pale Manchester City kwenda Borussia Dortmund Agosti mwaka 2017, umeonekana kuwa na manufaa makubwa kwake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 amekuwa nyota anayeongoza kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ambako amefunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho 16 msimu huu pekee, huku pia akiwa akicheza mara kwa mara kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England kinachonolewa na kocha, Gareth Southgate.

Sancho ni mmoja wa wachezaji wanaotajwa kwamba watawika zaidi kwa siku za usoni duniani, amekuwa akihusishwa zaidi na kuwaniwa na United, huku pia Liverpool na Real Madrid zikionyesha nia ya kuitaka saini yake.

Lakini straika wa zamani wa mashetani wekundu hao, Saha, mshindi mara mbili wa taji la Ligi Kuu England pale Old Trafford, hana shaka kwamba atang'ara United.

Alipoulizwa na Stats Perform News kama atafiti pale, Saha alijibu: "Kwa uhakika kabisa, ndio.

"Ni mchezaji ambaye ana kiwango cha juu, ana kasi, akili na ubunifu. Amepata miguu mizuri ya mpira, stamina na ubora.

"Ni mchezaji mbunifu sana akiwa uwanjani na ndio aina ya wachezaji wanaohitaji katika soka la kisasa. Sasa ukiwa na vitu vyote hivyo, utang'ara popote."

# NEYMAR, MBAPPE HAWAONDOKI PSG

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR na Kylian Mbappe watabaki Paris Saint-Germain, mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo ya Ufaransa amebainisha.

Leonardo, mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Brazil ambaye ndio mkurugenzi wa michezo pale PSG, amesema hana sababu ya kuamini kwamba fowadi hao nyota wawili wataondoka wakati wa dirisha la usajili.

PSG imeamua kuwaachia mfungaji mwenye rekodi klabuni hapo, Edinson Cavani na nahodha, Thiago Silva, ambapo wote walikuwa na nia ya kuwabakisha, lakini Neymar na Mbappe wamebakia wenye thamani zaidi kwa klabu hiyo.

"Hakuna kinachotuambia sisi kwamba (hawatabaki)," amesema Leonardo.

"Bado wana miaka miwili kwenye mikataba yao, na tunafikiria zaidi nini kitatokea baada ya wao kuendelea kuwa na sisi. Tunataka kwenda mbele."

Akizungumza na jarida la Le Journal du Dimanche, Leonardo alibainisha kwamba mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa, Mbappe ndiye mwenye thamani kubwa zaidi klabuni hapo.

Nyota huyo wa zamani wa Monaco mwenye umri wa miaka 21 amekuwa akihusishwa na klabu nyingine ikiwamo Real Madrid na Liverpool, lakini PSG hawana mpango wa kumwachia aondoke hapo Parc des Princes.

"Yeye ndio majaliwa ya PSG. Hilo ndio ambalo kila mmoja anataka," amesema Leonardo.

Wote, Neymar na Mbappe mikataba yao inamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021/22.

# SPURS YAJIUNGA KUMWANIA THIAGO

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, anatajwa kuingia kwenye mbio za kuwania saini ya beki wa Paris Saint-Germain, Thiago Silva, licha ya kuwapo na ushindani.

Nahodha huyo Mbrazil anatarajia kuondoka kwa mabingwa wa Ufaransa akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kumalizika mwezi huu na tayari yuko kwenye rada za Arsenal na Everton.

Mourinho anahitaji kumsajili beki huyo mwenye umri wa miaka 35 kutua hapo White Hart Lane ili kuchukua mikoba ya Jan Vertonghen ifikapo majira ya joto, liniandika gazeti la The Sun.

Silva amecheza mechi 30 za mashindano mbalimbali chini ya Kocha, Thomas Tuchel kabla ya msimu huu kusimama kutokana na janga la ugonjwa wa corona.

PSG imefuzu kutinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwafunga Borussia Dortmund kwenye hatua ya 16 bora.

Mkurugenzi wa Michezo wa PSG, Leonardo, ametangaza kuwa Silva hatapewa mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo na kumruhusu kwenda kucheza katika klabu nyingine yoyote ya Ulaya.

Tottenham ni moja kati ya klabu za Ulaya ambazo zinataka kumsajili Silva, ambaye anatajwa kuwa mmoja wa mabeki bora ambao wameichezea Brazil.

Everton na Arsenal pia nazo ziko kwenye mbio za kuwania saini ya beki huyo mwenye umri wa miaka 35 ili kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Mikel Arteta anajipanga kuimarisha safu yake ya ulinzi huku akijiandaa kuwaondoa kikosini kwake Shkodran Mustafi na Sokratis Papastathopoulos ili kutunisha mfuko wake wa fedha.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AUBAMEYANG BADO ANAIVURUGA ARSENAL

Ni kutokana na kugoma kusaini mkataba mpya kwa kutaka kujua hatima yake, huku vigogo wengine Ulaya...

**LONDON, England**

PIERR -Emerick Aubameyang amewapa changamoto Arsenal ya kuthibitisha kwanini anakataa kusaini mkataba mpya, akisema washikabunduki hao "wanashikilia funguo" juu ya majaliwa yake ya baadaye.

Nahodha huyo wa Arsenal anaingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wa kuitumikia klabu hiyo ya dimba la Emirates, huku mazungumzo kuhusu mktaba mpya yakiwa yamesimama.

Aubameyang amekuwa mchezaji muhimu kwa Arsenal tangu alipojiunga nayo akitokea Borussia Dortmund Januari, mwaka 2018, akifunga mabao 49 kwenye Ligi Kuu Englang katika mechi 75 alizocheza.

Lakini straika huyo wa kimataifa wa Gabon bado hajabeba taji na Arsenal na Aubameyang, ambaye amekuwa akihusishwa na timu kama Manchester United, Real Madrid na Paris Saint-Germain, amedokeza malengo ya kubeba mataji lazima yafikiwe kabla ya kusaini mkataba mpya.

"Hivi karibuni sijapata ofa yoyote ya kuongeza mkataba," amesema akiiambia Telefoot. "Lakini, bila shaka, tumekuwa na majadiliano na klabu kwa miezi michache sasa.

"Wanajua vizuri tu kwanini hakuna kilichotokea hadi sasa. Wao wana funguo. Ni juu yao wenyewe kufanyia kazi, baada ya hapo tutaona namna gani vitu vinakwenda.

"Ni muda wa kumaliza kipindi changu cha uchezaji, na nitakuwa mkweli kwa kila mmoja. Kwa namna fulani itakuwa ni uamuzi mgumu kuchukua. Bado sijaamua na tutaona. Pengine yatakuwa maamuzi muhimu zaidi katika kipindi changu cha uchezaji.

"Wachezaji wote wanataka kushinda mataji. Hivyo nataka kuhakikishiwa kwanza malengo haya."

## KWA UFUPI

**UNITED YAMGANDA GREALISH**

MANCHESTER United inatarajia kuongeza nguvu katika mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24), kwa dau la pauni milioni 75 baada ya kuelezwa isubiri miezi 12 ili kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20). ***(Star)***

**SANCHO AITAJA CITY**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (20), amesema atapendelea kurejea katika klabu yake ya zamani ya Manchester City kama Manchester United itakataa kulipa dau la pauni milioni 115 ambazo zimetakiwa na Borussia Dortmund. ***(Sun)***

**ALONSO ANUKIA NEWCASTLE**

NEWCASTLE United imeweka wazi nia yake ya kumsajili beki wa Chelsea Mhispania Marcos Alonso (29), ambaye hatima yake ndani ya Stamford Bridge haieleweki huku The Blues wakihusishwa na mpango wa kumnasa beki wa Leicester City, Ben Chilwell, 23. ***(Sun)***

**LEVERKUSEN YAKOMAA**

CHELSEA imesema iko tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 75 ili kumsajili kiungo, Kai Havertz (21), lakini klabu yake ya Bayer Leverkusen imesema inahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 90 ili kumuuza nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani. ***(Express)***

**NDIDI AGOMBEWA ULAYA**

MANCHESTER United imemweka kiungo wa Leicester, Wilfred Ndidi (23), katika orodha ya wachezaji inaowahitaji katika kipindi cha uhamisho, huku Real Madrid na Paris St-Germain pia zimeonyesha nia ya kumnasa mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria. ***(Express)***

**PARTEY AKARIBIA ARSENAL**

ARSENAL imetakiwa kumsajili kiungo Mghana, Thomas Partey, na tayari Atletico Madrid imekubali kumruhusu nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 kuondoka klabuni kwake. ***(COPE, via Caught Offside)***

**ARSENAL YAMFUATA KLUIVERT**

ARSENAL imeweka wazi inataka saini ya mshambuliaji wa Roma, Justin Kluivert (21), ambaye ni mtoto wa nyota wa zamani wa Uholanzi, Patrick, kama sehemu ya usajili wa Henrikh Mkhitaryan (31), ambaye yuko kwa mkopo katika klabu hiyo ya Serie A. ***(Gazzetta Dello Sport, Via Mail)***

**SPURS, ARSENAL VITANI**

KLABU ya Tottenham imetangaza nia ya kumsajili beki Mbrazil Thiago Silva ambaye ana umri wa miaka 35 ifikapo majira ya joto atakapokuwa mchezaji huru. Spurs itakumbana na ushindani kutoka kwa Arsenal na Everton. (Sun)

**DISASI ATAJWA ARSENAL**

ARSENAL imeanza mchakato wa kuwania saini ya nyota wa Reims, Axel Disasi (22), baada ya kubaini itakuwa na wakati mgumu wa kumnasa beki Mfaransa, Dayot Upamecano (21), kutoka RB Leipzig, kwa sababu ya dau lake kuwa juu. ***(Goal, via Express)***

**LOPEZ KUTUA ENGLAND**

TOTTENAHM Hotspur, West Ham na Chelsea zimeonyesha nia ya kuhitaji huduma ya golikipa Mhispania, Pau Lopez (25). Roma imetangaza kumuuza mlinda mlango huyo wa dau la pauni milioni 36. ***(Estadio Deportivo - in Spanish)***

**FORSTER ANUKIA CHELSEA**

CHELSEA imeweka wazi ina mpango wa kumsajili golikipa wa Southampton na Timu ya Taifa ya England, Fraser Forster, ambaye ana umri wa miaka 32. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# KICHUYA AFUNGA GOLI BARA IKIPITA MIEZI 26

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Shiza Kichuya amefunga bao la kwanza katika ligi hiyo baada ya miezi 26, imefahamika.

Bao la dakika ya 11 lililofungwa na kiungo huyo kwenye Uwanja wa Taifa dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara juzi, ndio bao lake la kwanza msimu huu, baada ya kurejea klabuni hapo.

Mara ya mwisho Kichuya kufunga bao ilikuwa ni Februari 26, mwaka 2018 kwenye uwanja huo huo jijini Dar es Salaam akiwa na timu yake ya Simba illipocheza dhidi ya Mbao FC, mechi ya Ligi Kuu msimu wa 2017/18.

Kwenye mechi hiyo, Kichuya alifunga bao la kwanza dakika ya 37, Simba ikishinda mabao 5-0, mengine yakifungwa na Emmanuel Okwi aliyepachika mawili, Erasto Nyoni na Nicolaus Gyan.

Ni msimu ambao kiungo huyo alimaliza akiwa na mabao saba ya kufunga.

Januari 2019, Simba ilimuuza kiungo huyo katika klabu ya Pharco ya Daraja la Pili nchini Misri ambayo nayo ilimtoa kwa mkopo kwenye klabu ya Ligi Kuu nchini humo ENPPI.

Hata hivyo hakuwa kwenye wakati mzuri nchini humo na Simba ilimsajili tena kwenye kipindi cha dirisha dogo msimu huu.

Pamoja na kusajiliwa alionekana kutokuwa kwenye kiwango kizuri, kiasi cha kukosa namba kwenye kikosi cha kwanza cha vinara hao wa Ligi Kuu Bara.

Kichuya alianzishwa kwenye mechi ya Jumapili dhidi ya Ruvu Shooting na kuonyesha kiwango kizuri kiasi na kufunga bao lake la kwanza na kwa klabu yake, ingawa baadaye alitoka na kumpisha, Francis Kahata kwenye mechi ambayo iliisha kwa sare ya bao 1-1.



Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, akicheza gofu katika mchezo maalumu wa kumuaga, Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Michael Dunford, uliofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mayanga afurahia kuidhibiti Simba

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuibana Simba, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Salum Mayanga, amesema wachezaji wake walifanya kazi nzuri katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Mayanga aliliambia gazeti hili shukrani za pekee anazipeleka katika safu ya ulinzi ambayo ilikuwa makini na iliwazuia washambuliaji wa Simba kutumia nafasi za kufunga walizotengeneza katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema wachezaji wake walifanikiwa kufuata maelekezo aliyotoa kwa kiwango cha juu hasa katika idara ya ulinzi na kiungo.

Alisema waliingia uwanjani wakiwa wanawaheshimu Simba kulingana na ubora wa kikosi chao na kufanikiwa kutumia vizuri nafasi ambayo walipata iliyotokana na uzembe wa mabeki zake.

"Simba wamecheza vizuri sana, baada ya kufungwa bao la kwanza, niliongea na mabeki wangu kuhakikisha wanaziba njia zote ambazo wapinzani wetu wangepata nafasi ya kutufunga, wakatekeleza," alisema Mayanga.

Hata hivyo, Mayanga alisema anajipanga kuyafanyia kazi mapungufu aliyoyaona katika mchezo huo ili yasijirudie kwenye mchezo wao unaofuata dhidi ya KMC FC ambao utaochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

## Azam yatangaza kumwacha Ngoma

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI uongozi wa Azam FC ukitangaza kuachana na mshambuliaji wake, Donald Ngoma, wachezaji wawili wa kimataifa, Bruce Kangwe na Never Tigere waliokuwa wamekwana kwao Zimbabwe wamewasili nchini jana, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin, 'Popat' alisema klabu hiyo imeachana rasmi na Ngoma ambaye mkataba wake wa kuwatumikia mabingwa hao watetezi wa michuano ya Kombe la FA, ulikuwa unamalizika juzi.

Popat alisema wachezaji waliobakia ambao hawajajiunga na kikosi ni kutoka Ghana na hiyo imesababishwa na masharti magumu ya nchini kwao.

"Kangwe na Tigere wameingia leo (jana), ila wachezaji wetu kutoka Ghana wapo katika 'lockdown', hivyo wanaendelea kuvumilia Kwa nyota hao hadi hapo masharti ya nchi yatakapowekwa sawa," alisema Popat.

Wakati huo huo, kocha wa timu hiyo, Aristica Cioaba, alisema nyota hao watakapokuja hataweza kuwatumia katika michezo ya hivi karibuni hadi hapo watakapokuwa fiti.

"Ni vigumu wachezaji hao wa kimataifa kuwahi michezo ya mwanzo katika ligi, hadi hapo watakapokuwa fiti," alisema Cioaba.

## Mkude aanza kujiweka imara

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba, Jonas Mkude, ameanza mazoezi mepesi ya kutembea kwa kuzunguka uwanja chini ya mtaalamu maalumu wa benchi la ufundi la timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam jana.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, ameliambia gazeti hili kiungo huyo ameanza mazoezi ya kutembea na leo ataangalia uwezekano na kumpa programu nyingine ya mazoezi kwa lengo la kumweka imara zaidi.

Sven alisema kutokana na majeruhi aliyoyapata katika mchezo wa kirafiki dhidi ya KMC, na kutakiwa kukaa nje kwa muda wa wiki mbili, lakini anafurahi kuona hali yake inaimarika mapema.

"Mkude anaendelea vizuri ameanza mazoezi ya kutembea leo (jana) asubuhi, nitaangalia baada ya hapo nina imani haitafikia muda huo uliopangwa na kuanza mazoezi ya ushindani," alisema Sven.

Alisema ana imani Mkude atarejea katika hali yake ya kawaida mapema na kuanza kutekeleza majukumu yake ya kusaidia timu hiyo kufikia malengo.

Kutokana na majeraha ya mguu aliyopata, kiungo huyo mkongwe wa Simba aliukosa mchezo dhidi ya Ruvu Shooting uliochezwa juzi jijini na kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Michezo
Jumanne Juni 16, 2020
Nipashe



Aubameyang bado anaivuruga Arsenal

HABARI UK 22





Mshambuliaji wa Simba, Ibrahim Ajibu (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Transit Camp katika mchezo wa kirafiki uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam jana. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA SC YAKATAA KUTUPIANA LAWAMA

●●●Ni baada ya kulazimishwa sare na Ruvu Shooting, kocha asifia ubora wa Maafande...

**Na Faustine Feliciane**

PAMOJA na sare ya bao 1-1 waliyoipata juzi dhidi ya Ruvu Shooting kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema timu yake ilijitahidi kupambana, lakini wapinzani wao walikuwa katika ubora wa hali ya juu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sven alisema hakuna anayepaswa kulaumiwa kutokana na matokeo ya mchezo huo ambao uliifanya timu yake iongeze pointi moja.

Sven alisema kuwa matokeo hayo waliyoyapata ni ya kawaida kwenye mchezo wa soka, hivyo kwa sasa wanaangalia na kuweka nguvu kuelekea mchezo unaofuata.

"Wachezaji walipambana kupata ushindi lakini matokeo yamekuwa kama yalivyo, hakuna haja ya kumlaumu mchezaji yoyote, mashabiki lazima waelewe matokeo kama haya yanatokea kwenye mpira, nimewataka wachezaji wangu sasa kuelekeza mawazo yao kwenye mchezo ujao," alisema Sven.

Mbelgiji huyo alisema kuna upungufu mdogo ambao aliuona katika mchezo huo kwa baadhi ya wachezaji, na tayari ameanza kuyafanyia kazi ili yasijirudie.

"Ni mapungufu madogo madogo ambayo naamini kwenye mchezo ujao hayawezi kuonekana, tutarejea kwenye mstari wetu wa ushindi katika mechi zijazo," aliongeza.

Kocha huyo alimsifia winga, Shiza Kichuya kwa kuonyesha kiwango kizuri katika mchezo huo, licha ya kuifungia Simba bao la utangulizi, ambalo Ruvu Shooting walifanikiwa kusawazisha.

"Alicheza vizuri sana na alitimiza majukumu niliyompa, taratibu atarejea kwenye kiwango chake cha juu, binafsi nafahamu ana uwezo mkubwa na ni mchezaji ambaye anaweza akakufanyia kile ulichomtuma," Sven alisema.

Simba ambayo imeshuka dimbani mara 29, inaendelea kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 72 ikiwa na tofauti ya pointi 18 dhidi ya Azam FC iliyoko nafasi ya pili baada ya kujikusanyia pointi 57 na Yanga yenye pointi 54.

Hata hivyo Yanga ambayo pia inafundishwa na kocha raia wa Ubelgiji, Luc Eymael ina mchezo mmoja pungufu.

Katika kuendelea kujiimarisha, jana asubuhi Simba ilicheza mechi nyingine ya kirafiki dhidi ya Trans Camp na kuibuka kwa ushindi wa mabao 4-0.

Simba itashuka tena uwanjani Jumamosi kuwakaribisha Mwadui FC kutoka mkoani Shinyanga, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

## Morrison ageuka gumzo bungeni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Yanga, Bernard Morrison, jana, alizua gumzo baada ya timu hiyo kutinga bungeni huku Spika wa Bunge, Job Ndugai akisema wabunge wanamuulizia Mghana huyo.

Morrison hakuwa katika kikosi cha Yanga kilichokwenda Shinyanga kuwavaa Mwadui, na sasa timu hiyo iliwasili jijini hapa kwa lengo la kuwakabili wenyeji, JKT Tanzania katika mchezo mwingine wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Ndugai aliwahakikishia wabunge kuwa endapo Simba na Yanga zitakutana tena, basi mabingwa na vinara wa Ligi Kuu, Wekundu wa Msimbazi wataibuka na ushindi.

Akitambulisha timu hiyo jana bungeni, Ndugai aliuliza mchezaji huyo amekaa wapi katika eneo la wageni.

Ndugai alisema "Ninawageni kwenye gallery yangu (sehemu ya kukaa wageni), kwenye gallery ya Spika ni viongozi wa Yanga naomba wasimame, gallery yangu ya kulia ni wachezaji wa Yanga na baadhi ya viongozi wa timu ya Yanga, karibuni sana hapa bungeni, tunafurahi sana kuwa nanyi, hili ni bunge lenu sasa mnaweza mkakaa."

Hata hivyo, Ndugai alihoji alipo mchezaji huyo kwa kuwa wabunge wanamuulizia na kuwataka wabunge ambao ni mashabiki wa timu ya Simba wawashangilie Yanga.

"Wabunge wanauliza mchezaji mmoja tu sijui Morrison naomba asimame Morrison yupo, yupo? Hayupo, naomba wale waheshimiwa wabunge wa Simba wapeni makofi kidogo," alisema Ndugai.

Aliongeza licha ya Simba kufungwa katika mchezo uliopita kwa bao 1-0, lakini watakapokutana tena wanauhakika Simba itaibuka mshindi.

Alisema Yanga isisahau ushindi huo bado wanaukumbuka.

"Ule mkuki mmoja, ule bado tunaukumbuka sana tutakapokutana tena mjiandae kisawasawa maana itarudi mikuki kadhaa," alisema Ndugai huku akishangiliwa na wabunge.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >